


SAUTIZETU

maelezo na habari



MAELEZO NA HABARI



SAUTIZETU

MAELEZO NA HABARI

ISSUE V | 2013

JAMII WAZI YA MPANGO WA AFRIKA MASHARIKI (OSIEA)

mkurugenzi mkuu BINAIFER NOWROJEE

wahariri EMMA DAY
JOSHUA LUBANDI
BINAIFER NOWROJEE
UMRA OMAR

mkurugenzi ubunifu ASSEGID GESSESSE
mkurugenzi sanaa ISSA ABDUL

waandishi JACOB AKOL
EMMA DAY
HEATHER DOYLE
JEGGAN GREY-JOHNSON
MAXWELL KADIRI
GASTA KAKAIRE
DAVID MAKALI
BOAZ MUHUMZA
UMRA OMAR
NATHAN ONYANGO
JOANNA OYEDIRAN
RACHEL THOMAS

tafsiri NICODEMUS MINDE

TOVUTI NA MAONI

www.osiea.org | info@osiea.org

OSIEA INACHUKUA JUKUMU KUBWA KATIKA
KUHAMASISHA MIJADALA YA WAZI NA YENYE UFAHAMU
KUHUSU MASWALA YALIYO/YA MUHIMU MIONGONI
MWA UMMA YA AFRIKA MASHARIKI

NAIROBI | KAMPALA | DAR ES SALAAM | JUBA

Imechapishwa na:

OSIEA

S.L.P 2193-00202

Nairobi, Kenya

+254 (20) 387-7508

© OSIEA.

Pasipokuwa na viziuzi, unaweza kuchapisha tena kazi yetu. Shirika la OSF linaamini kwamba lengo lao linaendelezwa endapo kazi tunazozisaidia na kubuni zinawekwa wazi na zinapatikana kwa umma.

TAHARIRI

Tunaishi katika dunia ya teknolojia ambayo ni ya haraka, ndogo na safi, ambapo mawazo yanawasilishwa katika spidi kali na kupitia majukwaa tofauti tofauti. Huku kuleta watu, jamii, na mataifa kumefungua na kutengeneza njia za maelezo na taarifa kote ulimwenguni jambo ambalo halikudhaniwa hapo awali. Hakuna kipimo cha uwanda na upeo wa taarifa.

Ama kuna kipimo?

Kwa njia mbali mbali, taarifa na maelezo yanazidi kugandamizwa licha ya upanuzi wa wigo la taarifa. Wakati mwingine, unyamazishaji wa nguvu wa serikali kupitia sheria na hatua gandamizi huzuia sauti za wananchi. Ofisi za serikali Afrika Mashariki zinaendeshwa kupitia utamaduni wa siri badala ya msingi wa kuwa na taarifa za umma ambazo kwa kiasi kikubwa lazima ziwe zinapatikana. Katika hatua nyingine, vyombo vya habari vinajisitiri vyeneyewe katika masuala fulani yaliyo nyeti ama masuala tete kama usalama wa kitaifa ama wizi wa kura, kwa woga. Giza hili la taarifa haipo tu kwa vyombo vya habari. Watu walio na ulemavu wa hisia fulani wanalazimika kuishi katika dunia iliyopungufu ya lugha ya ishara, Braili na huduma za ukalimani ilikuwajumuisha kikamilifu katika jamii. Nyenzo za kisasa pamoja na jukwaa za ujumbe mfupi (arafa) yana uwezo mkubwa wa kuzifikia jamii zilizotengwa ilikutoa taarifa, kuwashirikisha na kuwaandaa.

Jamii Wazi ya Mpango wa Afrika MASHariki (OSIEA), kwa ushirikiano na mipango mingine katika shirika la Open Society Foundations, linafuraha kufanya kazi na washirika kadha wa kadha ambao hupata njia kupanua mipaka ya umma na kuleta fikra muhimu.

Hakika kuna njia nyingine bora ya kujenga jamii iliyochangamfu kuliko taarifa katika mfumo mzuri wa upatikanaji ili watu waweze kushiriki na kufanya maamuzi bora katika masuala yaliyo muhimu katika maisha yao?

Binaifer Nowrojee

Binaifer Nowrojee
Mkurugenzi Mkuu



KATIKA

4
Tahariri

8
Redio nje ya
Studio

12
Uvumbuzi unapokutana
na Utawala

16
Giza la Taarifa:
Watu wenye
Ulemavu wa Hisia

20
Ukuaji wa Matumizi ya Tovuti
za Habari Nchini Sudan

24
Midahalo hufanya
Wananchi kuwa Mahiri

26
Waandishi Habari katika
Mstari wa Moto

TOKEO HILI

Kutafuta Mazungumzo kupitia
Sanaa na Utamaduni

30

Makosa katika Vita
Dhidi ya Ugaidi

34

Wauza Ngono katika Mstari
wa Mbele wa kutumia Ujumbe
Mfupi (SMS)

38

Mwito wa Kimya wa
Uwajibikaji Katika
Uandishi Habari

42

Kutoka Vyombo vya
Habari vya Kitaifa hadi
Uhuru katika Utangazaji


46

Afrika ina Haki
ya Kujua

48

Kuondoa Dhana Potofu ya
Vyombo vya Habari

50



redio^{nje} ya studio

NA EMMA DAY



**KATIKA MAENEO YA KIJIJINI,
REDIO INAKUWA CHOMBO
MUHIMU CHA JAMII KUELEZA
MASAIBU YAO NA KUITISHA
MABADILIKO**

Kaskazini Uganda ni moja wapo ya maeneo yaliyo magumu sana kufikia watu, hususan akinamama, kupitia mifumo asili ya vyombo vya habari, kama ilivyoielezwa na shirika la mawasiliano la Panos East Africa. Baada ya miongo miwili ya vita, eneo zima limekumbwa na majanga na miundombinu imedhoofika kabisa. Familia zinataabika kupata maji, chakula, usafiri, na makazi, sembuse televisheni na magazeti, hivyo wengi wao hutegemea redio kupata habari. Hata hivyo, nchini Uganda, asilimia 80 ya vituo vya redio vinamilikiwa na wanasiasa kutoka kwenye chama tawala ama wafanyabiashara waliokaribu na chama tawala.

Wakati wa vita, idadi kubwa ya watu wa Kaskazini Uganda walivurumishwa makwao kutokana na machafuko ama kuamishwa kwenye kambi zilizoundwa na serikali ili kuwalinda na kundi la waasi la Lord's Resistance Army (LRA). Wakati wanaume walipolazimishwa kupigana dhidi ya LRA, idadi kubwa ya familia zilibaki kuongozwa na akinamama. Akinamama wakabaki kuwa watafutaji na walezi wa familia. Vita ilipoisha, familia zikaanza kurudi kwenye mashamba yao na kujenga maisha yao, ila kutokana na kuharikibika kwa sehemu kubwa ya maisha yao, mambo hayakurudi kama hapo awali.



ILA UNAONA WANAWAKE WAKISIMAMA NA KUZUNGUMZA NA KUWA HODARI NA KUZUNGUMZA MASUALA YAO

Kutokana na msongo wa mawazo na hali ya kuhisi kama huwezi kufanya kitu kutokana na kukosa ajira, idadi kubwa ya wanaume wamegeukia pombe na kuanza kuwapiga wake zao na watoto, na kufuja mali ya familia. Mipango kadhaa ipo njiani Kaskazini Uganda kusaidia watu wapate makazi yao upya.

Hapo awali mume wangu angeuza shamba bila kushauriana nami. Angeuza shamba letu na kutumia hela hizo kulewa. Lakini tulipojiunga kwenye kikundi cha akinamama, tulielimishwa kuhusu haki zetu za mashamba na umuhimu wa kujadiliana na wenza wetu. Hivi karibuni alipotaka kuuza shamba, tulikaa chini pamoja na kujadiliana kuhusu bei pamoja na kujua thamani yake pamoja na watoto wetu na tukatumia fedha zile kuwapeleka watoto wetu shule. Kwasasa najihisi kama mwanamke nina haki ya kusikilizwa na uhusiano wetu umeimarika.

- Agoro Santina, mwanachama wa Kikundi cha Akinamam wa Mon Pae Yot (FOKAPAWA)

Chombo cha habari mahiri kupitia mfumo wa redio ya kijamii kimeibuka katika eneo hili, ambacho kina zaidi ya stesheni kumi za redio. Vituo hivi vya redio, vikitangaza katika lugha asili ya Kiluo, vimekuza midahalo ya umma kuhusu haki za kibinadamu, uwazi na uwajibikaji katika utawala, na uhusiano wa kinyumbani. Matangazo ya redio yamekuwa nguzo kubwa ya kuwakutanisha tena wakinamama waliotekwa nyara na familia zao.

Shirika la Panos limeanzisha mbinu bunifu za kuleta redio karibu na jamii zilizopo vijijini ambazo kwa miaka mingi zimetengwa nchini na kutengwa na mifumo yote ya vyombo vya habari. Shirika la Panos limekuwa likifanya kazi kwa ushirikiano na vituo vya redio vijijini kuwafikia jamii ya Wakaramoja ambao hawasikiki na huishi vijijini. Jamii hii ni ya wafugaji na huishi kaskazini-mashariki Uganda. Kupitia mpango huu, Shirika la Panos lilitoa mafunzo kwa waandishi wa habari wa huko, wakawapa pikipiki ili wasafiri hadi vijijini, na kanda zilzorekodiwa. Kwa mara ya kwanza redio ilitoka studio. Hapo awali akinamama walitengwa katika midahalo, ila kwasasa wamepata sauti zao na redio hatimaye imetoka studio na kufika maeneo ya vijijini.

Wasikilizaji kwasasa wanataka vipindi hivi viendeleo kwasababu vimekuwa nyenzo kuu kwao.

Watangazaji wa redio Panos wameenda hadi Karamoja kujadili masuala yaliyo muhimu kwa wananchi wa eneo hilo, pamoja na kuzungumzia masuala ya matumizi ya mashamba, dhuluma za nyumbani, dhuluma za kimapenzi, na upa-

tikanaji wa maji na ardhi. Wanahimiza akinamama washiriki kikamilifu katika midahalo, na kutaja masuala yaliyo na umuhimu kwao. Mjadala hii hurekodiwa, na huletwa studio na hurushwa redioni. Kando kando ya matangazo haya, Panos huwaalika wazee wa mtaa kujibu maswali moja kwa moja hewani na kushiriki ndani ya studio pamoja na simu za moja kwa moja kutoka kwa wananchi.

Panos wanasema *“kupitia kwa mjadala ya kijamii akinamama wametaja masuala kadhaa, wanaume wamewasikiliza, wam-etekahisia za waunda sera na hii imesaidia kuleta mabadiliko”*.


Mojawapo wa mafanikio inajumuisha kituo cha afya katika wilaya ya Pader Kaskazini Uganda. Kituo hicho cha afya hakikufunguliwa kwasababu muhudumu wa afya aliyepangwa hapo alipendelea kuba ki mjini kuliko kuja Pader na kutibu wagonjwa. Katika kisa kimoja, mama mjamzito alikuja katika kituo hicho cha afya na kukuta hakuna mtu wa kumhudumia, hatimaye alifariki kutokana na matatizo ya mtoto ambayo yangeweza kuepukika. Kituo cha redio hapo, Luo FM, kilifuatilia kisa hicho na kijadili mikasa waipatayo akinamama na hali ya uozo wa huduma za afya katika eneo hilo. Mjadala huo ulirushwa kwenye redio ya hapo, na wazee wa mtaa waliletwa kwenye kipindi kujibu maswali kuhusu hali duni ya huduma za afya. Kwa matokeo hayo, muhudumu wa afya akabadilishwa.

Kupitia mjadala mwingine katika eneo la Kitgum uliorushwa na Mighty Fire FM, wakinamama waliweza kudai haki zao za

kiuchumi, kwa kujadili na wanaume. Serikali inatoa mzunguko wa fedha katika eneo hilo kuwasaidia wanaume na akinamama Kitgum, ila wanaume hawakuwajumuisha akinamama katika mzunguko huu wa fedha. Mjadala huu katika redio uliweka ulingo mzuri kwa wanawake kuwashawishi wanaume kuwa ni lazima nao wajumuishwe katika mzunguko huu, ambao kwasasa upo wazi kwa wote wanaume na wanawake. Mafanikio haya yamesaidia kuwawezesha akinamama kutambua hali zao za kuhusishwa katika kufanya maamuzi ambayo yanawagusa.

Lucy Atim, zamani akiwa Panos East Afrika, anasema, *“Inafurahisha kuona mabadiliko ambayo mnaifanya kwa kutengeza jukwaa kwa watu kujadili. Wakati mwingine mabadiliko huja pole pole, ila unaona wanawake wakisamama na kuzungumza na kuwa hodari na kuzungumza masuala yao, pia kwa wanaume kukaa na kusikiliza na kuhoji na kujadili pamoja na akinamama, kwa jamii kuja pamoja na kujadiliana. Umekuwa mchakato uliyozaa matunda.”*

Emma Day ni mwanasheria wa kujitegemea wa haki za kibinadamu.





UVUMBUZI UNAPOKUTANA NA UTAWALA

NA EMMA DAY



**KUWALETA WANANCHI
WA AFRIKA MASHARIKI
KUJADILI MATUKIO YA
KILA SIKU SIO KUGUMU
ENDAPO KIPINDI
CHA TELEVISHENI
KINAFANYA HIVO KWA
KUTOA BURUDANI KWA
WATAZAMAJI**

Nchini Tanzania mamilioni ya wananchi wa kawaida husafiri kuelekea kazini kwa usafiri wa mabasi madogo ama kupitia mradi wa kuelimisha jamii wa minibuzz, mashuhuri kama daladala, Kila siku basi dogo maalum lenye muundo wa daladala husimama kwenye kituo cha mabasi na hubeba kundi la abiria bila mfuatilio wowote na kuwapa usafiri wa bure kuelekea kazini. Mabasi haya (minibuzz) lina vyombo vya kuchukua video na watangazaji wachangamfu ambao huwaalika abiria kujadiliana kuhusu matukio ya kila siku wakielekea kazini. Abiria hucheka, hulumbana, hubishana na hufurahia, wakati wanapojadiliana kwa nguvu, na mazungumzo yao ya asubuhi hurushwa kwenye kipindi cha usiku kwenye televisheni kuanzia saa 12 jioni.

Wakati wa mjadala kwenye minibuzz kuhusu mchakato wa kuandika katiba mpya Tanzania, Daniel ambaye ndiye mtayarishaji wa kipindi, huuliza "Katiba kwanza ni nini?" Abiria wa kiume hujibu, "Ndiyo sheria mama nchini. Ndiyo mhimili wa kila kitu." Abiria wanaafikiana kwamba katiba ni ngumu sana kwa mwananchi wa kawaida kuchangia ama hata kuelewa.

Mwanaume mmoja anamaka: "Kwa ufupi hatujui chochote kuhusu katiba. Ukiachilia wanasiasa na wasomi wachache kwenye jamii...shida zenu zote, ufidadi, ufujaji wa mali za nchi, wewe zitaje, zote hizi husababishwa na mapungufu katika katiba yetu ya sasa...Ila katika nchi nyingine kuna utofauti kidogo. Mawaziri huwajibika kwasababu katiba zao huwalazimu hivyo.

Daniel anamuuliza abiria wa kike maoni yake kuhusiana na suala hili. Anasema, "Kama serikali inasikiliza...". "Hakika wanasikiliza!" Daniel anaingilia kati. Mama yule anaendelea, "Lazima wahusishe mashirika ya kiraia kwa nguvu kama wafanyavyo wakati wa kampeni za siasa. Sio wote wanauwezo wa kupata magazeti. Sio wote wanaweza kupata redio ama televisheni...Lazima watumie nguvu kama vile wanavyotumia wakati wa uchaguzi!"

Daniel yuko sahihi kusema kwamba serikali inasikiliza. Mpango wa minibuzz umeteka masikio ya waunda sera, na watangazaji walialikwa bungeni kukutana na mawaziri kutokana na mafanikio ya kipindi hicho na uwezo wake wa kuwapa sauti wananchi wa kawaida.

“

UFANISI KATIKA VIPINDI
HIVI BUNIFU VYA
TELEVISHENI NI UWEZO
WAO WA KUBEBA UJUMBE
MZITO



Nchini Kenya, kampuni ya filamu ya Medeva ilianzisha kipindi cha Ajenda Kenya, kipindi cha maongezi kilichopata sifa na tuzo, ambacho kilikuwa kipindi cha kwanza kabisa cha maongezi nchini. Jopo la wachangiaji lilijumuisha watoa maoni mbali mbali, wataalamu na maafisa wa ngazi ya juu serikalini, pamoja na wengine wengi.

Wakati ule Medeva ilipoanzishwa, palikuwa na haja ya kuwawezesha waandishi wa habari nchini washiriki katika mijadala yao ya utawala. Medeva kwasasa wameshatoa mafunzo kwa waandishi wa habari 400 kutoka Kenya na Uganda kwenye utaalamu wa utayarishaji wa vipindi redioni na kwenye televisheni, kwa lengo la kukuza utawala wazi na maudhui husika kwenye ukanda huu. Kufuatia mfumo mpya wa ugatuzi, mpango sasa ni kufika zaidi maeneo mengi ya vijijini, ili watu waweze kuwawajibisha serikali za makaunti kwa ufasaha. Karibia watazamaji milioni 1.5 hutizama kipindi hiki maarufu kila wiki.

Shule ya mafunzo ya filamu na televisheni nchini Kenya ya Mohammed Amin ilianzisha na kurusha kipindi cha maongezi kilichoendeshwa na wanafunzi ambapo masuala ya haki za kibinadamu na masuala ya kijamii yalizungumziwa na watazamaji, waandaji wa kipindi, wataalamu na wananchi walioathirika. Kipindi hiki cha mazungumzo kilibuniwa na kuandaliwa na wanafunzi watatu wa mwaka wa pili mwaka 2005. Wanafunzi waliandaa vipindi vifupi maalumu kuhusiana na masuala ya kijamii ambayo kwa wakati ule yalijadiliwa na watazamaji moja kwa moja studioni katika eneo kubwa la miraba 300 likishiria mitaa ya jiji la Nairobi ambalo likawa utambulisho wa kipindi. Katika kipindi cha miaka mitano, vipindi 58 viliandaliwa na wanafunzi wa filamu na kuonyeshwa katika televisheni kuu za Kenya. Mada zilihusu

ulemavu wa ngozi, uongozi mbadala, unyanyasaji wa watoto, haki za kikazi, nishati mbadala, kufikiria upya elimu rasmi na haki za wauza ngono.

Kipindi cha mazungumzo cha HATUA TV kilikuwa nyenzo muhimu cha kujenga uwezo katika ukuaji wa sekta ya televisheni Afrika Mashariki; kutoa mafunzo ya haki za kibinadamu kwa wataalamu wa baadae wa televisheni; na chombo cha mabadiliko ya kijamii na mijadala nchini. Kufukia muhula wanne wa kipindi hiki, kilikuwa kimevuka hadi kuonyesha kwenye televisheni kuu, na kufikia takriban watazamaji milioni mbili Afrika Mashariki. Vikao hivi vilijumuisha jumla ya wanajopo elfu mbili kutoka sekta zote za jamii kuja pamoja na kuzungumza kwa uwazi haki zao, visa vyao na ufumbuzi wa matatizo yanayowakumba katika maisha ya kisasa nchini Kenya mbele ya watazamaji zaidi ya mia moja. Wote waliondoka studioni wakizungumzia yaliyojiri kwenye kipindi.

Pia nchini Kenya, katika kipindi cha XYZ (ambacho hivi karibuni kimeshinda tuzo ya mchezo bora wa televisheni Afrika katika tuzo za Africa Magic Viewers' Choice Awards) kwa ujuzi waliunda vikaragosi wakileta uhalisia wa kuiga wanasiasa nchini Kenya. Kwa matumizi ya ucheshi na kuvichezesha vikaragosi kipindi kinafanikiwa kufukia kiwango cha kukosoa serikali ambapo pasingewezekana kupitia mtazamo wa kawaida tu. Kipindi kimerushwa na Televisheni ya Citizen na pia hurushwa kwenye vituo kadhaa vya redio pamoja na kwenye mabasi ya Nairobi kupitia teknolojia ya runinga ya Roma LCD.

Kipindi cha XYZ kilianzishwa mwaka 2009 kama ushirikiano kati ya watayarishaji wawili; Gado ambaye ni mhariri wa katuni na mchoraji wa Nation Media Group; na Marie Lora-Mungai, ambaye ni mwandi-

shi wa habari, mwandishi na mtayarishaji, wakiiga kipindi kama hicho kilichoanzishwa nchini Ufaransa. Gado aliona uwezo wa kutumia dhana hio nchini Kenya, kuhabarisha kutumia ucheshi "uozo wa ufsadi na usimamizi mbovu wa nchi." Vituo vya televisheni nchini vilisita kukifadhili kipindi hicho, kwahivyo kampuni hiyo ya utayarishaji ilianzisha kampuni ambayo hatazamii faida ambayo hupata ufadhili kutoka nje. Kipindi cha XYZ kwasasa kinaaminika kimefika kiwango cha kumpendwa sana, na kinaufuatiliwa wa zaidi ya milioni saba kwenye televisheni, redio, mabasi na kwenye mitandao ya intaneti.

Ufanisi katika vipindi hivi bunifu vya televisheni ni uwezo wao wa kubeba ujumbe mzito, na kubaki katika hali ya kushirikisha kila mtu, kufurahisha na kupatikana kwa watazamaji wengi wa televisheni. Vipindi hivi huanika masuala ya ufsadi na kutokufuatwa kwa sheria kwa kuteka hisia za watu fulani ambao mara nyingi wangebadilisha kipindi cha televisheni endapo kungekuwa na mijadala ya kisiasa ambayo haina ladha, kwa kutumia mbinu bunifu na kuzipatia sauti matatizo ya wananchi wa kawaida.

Emma Day ni mwanasheria wa kujitegemea wa haki za kibinadamu

GIZA I A

TAARIFA

WATU WENYE ULEMAVU WA HISIA

NA BOAZ MUHUMUZA



**WALE WENYE ULEMAVU
WA KUONA, MABUBU
NA MABUBU-VIZIWI
HUIISHI KATIKA GIZA LA
TAARIFA KWASABABU
NYENZO ZA MAWASILIANO
HAZIJUMUISHI MIFUMO
YAO YA ULEMAVU**


Kwa watu walio na ulemavu wa hisia, taarifa ndio maisha kwao. Bila taarifa ambazo huwasilishwa kwa mfumo mzuri, kipofu ama kiziwi hawezi kushiriki na wenzake kika-milifu, ama kupata huduma za umma. Watu walio na ulemavu wa hisia (kama wenye ulemavu wa kuona, wenye ulemavu wa kusikia, na mabubu-viziwi) wanaishi katika giza la taarifa. Kila kundi la hawa hupata changamoto fulani kwasababu kuu ya njia na nyenzo za mawasiliano hazijumuishi mifumo yao ya ulemavu.

Viziwi hupata taarifa na kujieleza kupitia lugha ya ishara. Ijapokuwa nchi nyingi zimetambua rasmi lugha ya ishara, serikali chache sana hukuza matumizi yake

kwenye maisha ya umma. Hii moja kwa moja hudhuru maisha ya kila siku ya viziwi wakati mwingine hugusa maisha yao kwa undani, kama vile upatikanaji wa huduma mbalimbali. Mtu anayeweza kusikia ana uwezo wa kuingia na kuwasiliana na mhudumu wa afya wakati wowote kupata matibabu. Kiziwi lazima akodi mkalimali, jambo ambalo ni la kawaida, viziwi hupata shida kupata huduma za umma. Hata kwa usaidizi wa mkalimani kuna vikwazo vingi ambavyo huwakumba viziwi kujieleza kwa ufasaha. Kwa kuwa vituo vingi vya televisheni na vyombo vingine vya habari vimedharau matumizi ya lugha ya ishara katika taarifa zao za habari, viziwi huwachwa kwenye giza kuhusu habari zinazochipuka na habari za kila siku.

“

HATIMAYE, ULEMAVU HUWA
MIONGONI MWA JAMII
AMBAZO HAZIJITAHIDI
KUJUMUISHA UTOFAUTI WA
WALE AMBAO WANAUWEZO
TOFAUTI



Mahitaji ya waalemavu wa kuona hakika ni kinyume na haya. Kutokana na maendeleo katika teknohama, dunia kwasasa ni ya muono zaidi. Simu za viganjani na tarakilishi kwa sasa zinaendeshwa kwa kubonyeza tu jicho. Licha ya kuwa haya ni maendeleo chanya, mara nyingi huwatawaga walemavu wa kuona. Intaneti na simu zinakuwa vyanzo vya taarifa, wakati huo huo zikiwa jukwaa za kujieleza kijamii. Watu wenye ulemavu wa kuona wanapata shida kwenda unyo unyo na wenzao katika sekta hii. Tarakilishi na simu nyingi hazina programu za kusoma zilizojengwa pamoja na vidude hivi ambavyo vinaweza kutoa taarifa kwa njia ya sauti za walemavu wasio ona. Programu hizi zina gharama na huweza tu kuwekwa kwenye simu na tarakilishi maalumu. Njia za zamani za kupata taarifa pia hazina uafadhali. Nyaraka nyingi rasmi ambazo hupatikana kwa umma ni za kuchapishwa. Hii inahitaji mtu wa kumsomea nyaraka hizi za msingi kwa maendeleo ya matumizi ya dawa.

Viziwi-vipofu hutumia kugusa kama njia ya kuwasiliana ambapo taarifa hupitishwa kupitia kugusa kwa njia maalum mwili wa mtu. Serikali nyingi hazijaendeleza mafunzo ya lugha ya kugusa. Hakuna,

ama wapo waalimu wachache waliofunzwa kutoa mafunzo ya mawasiliano ya kugusa katika ukanda wa Afrika Mashariki. Matokeo yake, viziwi-vipofu hawawezi kupata elimu rasmi. Wanabaki kutengwa na dunia, wanashindwa kuwasiliana hata na wale waliokaribu nao sana.

Mkataba wa Umoja wa Kimataifa unao-shugulikia Haki za Watu wenye Ulemavu (CRPD), ambao umefanywa sheria na nchi nyingi hulazimu nchi kuhakikisha watu wenye ulemavu wanapata taarifa kupitia ukuzaji wa njia mbadala za mawasiliano kama vile Braili, lugha za ishara, lugha ya kawaida, na lugha ya kugusa pamoja na nyingine. Msingi wa lugha ya ishara lazima ujumuishwe kwenye mafunzo ya kitaalamu ya watoaji wa huduma za umma, kama vile walimu, wahudumu wa afya, maafisa wa polisi, ili kuwawezesha kuwasiliana na wateja walio na ulemavu wa kusikia. Serikali lazima itoe wakalimali kusaidia viziwi kupata huduma za umma. Taarifa zilizopigwa chapa lazima pia zitolewe kwa mifumo inayoweza kupatikana kwa walemavu wa kuona kama vile chapa kubwa, Braili ama nakala za kusikilizwa. Wahusika wakuu katika utengenezaji wa simu na tarakilishi lazima wahakikishe kwamba vifaa vya elektro-

niki vinawekwa programu za kusoma na kukuza maandishi ilikuwezesha walemavu wa kuona waweze kutumia. Serikali lazima pia ikuze ufundishaji wa Braili, lugha ya ishara na lugha ya kugusa kwa jamii husika ya walemavu ili kuwawezesha kupata taarifa.

Sheria ya kimataifa iko wazi ikieleza kwamba upatikanaji wa taarifa na haki ya kujieleza ni haki ambazo huwawezesha wananchi wote kudai taarifa kutoka kwa serikali zao. Na kwa uwazi kujieleza kulingana na masuala ya kitaifa. Hatimaye, ulemavu huwa miongoni mwa jamii ambazo hazijitahidi kujumuisha utofauti wa wale ambao wana uwezo tofauti.

Boaz Muhumuza ni afisa wa mradi wa haki ya walemavu wa Jamii Wazi ya Mpango wa Afrika Mashariki (OSIEA)



UKUAJI WA MATUMIZI

YA TOVUTI ZA HABARI

NCHINI SUDAN

NA JOANNA OYEDIRAN

Kutokana na ongezeko la vidhibiti wa vyombo vya habari na mdororo wa kiuchumi kwenye vyombo vya habari vya chapa, Wasudan wanabuni fumbuzi mpya za kutoa taarifa, kujadili mustakabali wa taifa lao na kufanya kampeni ya mabadiliko. Sudan kwa mshangao ina kiwango kikubwa katika upenyezi wa intaneti, kulingana na umoja wa kimataifa wa mawasiliano wa simu inakadiriwa kuwa, asilimia 10 ya wananchi wanaweza kupata intaneti kwa kuongeza, idadi kubwa wanapata intaneti kupitia simu za mkononi.

Kuna ongezeko la watumiaji wa tovuti za blogu, na idadi kubwa za hizi blogu zikitumiwa na wa Sudan waishio ng'ambo. Wimbi la hivi karibu la uoneaji wa vyombo vya habari na magazeti kufungwa

kumefufua hamu ya kuanzisha magazeti ya intaneti. Tovuti hizi zinaweza kukwepa uthibiti wa awali ambao magazeti mengi ya chapa yanalazimishwa kupitia mara kwa mara. Mwaka 2012, *al-Taghyeer* likawa gazeti jipya lenye tovuti, likiungana na *Sudanile*, *Sudan Tribute*, *Al Rakoba na Hurriyat Sudan*. Shirika la Kitaifa la Usalama na Kijasusi (NSIS) limefungia wahariri wa magazeti kutoa makala ya maandishi wengi wa *al-Taghyeer*, pamoja na mhariri mkuu. Tovuti za habari zinaainishwa kama za kisomi lakini kwa ukaribu sio kama yale magazeti ya chapa. Mtandao wa usamabazji wa magazeti unaenda mpaka nje kidogo wa jiji la Khartoum hadi miji midogo kwasababu ya changamoto za kifedha na usafirishaji. Usambazaji wa gazeti kuu la kila siku la *Al-Intibaha* inaaminika kuwa 60,000.



WASUDAN WANABUNI FUMBUZI MPYA ZA KUTOA TAARIFA, KUJADILI MUSTAKABALI WA TAIFA LAO NA KUFANYA KAMPENI YA MABADILIKO



NSIS ILIANZISHA KITENGO CHA` JIHADI YA KIMTANDAO` KUKAGUA INTANETI NA KUSUMBUA WANAHARAKATI


Kutokana na maendeleo haya, serikali ya Sudan imejaribu kuziba pengo katika jithada za kudhibiti upatikanaji wa taarifa kwa wananchi. Mwaka 2010, ilibainika kwamba NSIS ilianzisha kitengo cha` jihadi ya kimtandao` kukagua intaneti na kusumbua wanaharakati. Wakati wa maandamano Juni na Julai 2012, serikali ya Sudan iliwatia ndani na kuwazuia mwandishi Maha El Sanusi, na Salma al-Wardany, mtangazaji mmoja wa Misri anayefanya kazi na kituo cha Bloomberg. Salma al-Wardany hatimaye alifukuzwa nchini.

Tume ya Kitaifa ya Mawasiliano pia imefungia baadhi ya tovuti za habari na majadiliano. Hurriyat Sudan bado imefungiwa hadi sasa ila imeendeleza usomwaji ndani ya Sudan kwa kuwahimiza wasoma-

ji kuwapata kupitia mitandao ya kijamii kama Facebook na Twitter. Kufungwa kwa mitandao ya Twitter na Facebook, hususan Facebook ambayo inapendwa sana na Wasudan itakuwa hatua mbaya sana.

Mwaka wa 2012, maafisa wa serikali wa Sudan walitumia nguvu kubwa ya sheria dhidi ya bloga maarufu wa video Nagla Sidahmed na mwanaharakati wa kisiasa Jalila Khamis kufuatia kusambaza video moja kwenye mitandao ya mahojiano kuhusiana na athari za mgogoro unaondelea wa Kordofan Kusini. NSIS walimzuia Jalila na wakaendelea kumyanyasa Nagla, na kumlazimisha kutoroka Sudan pamoja na familia yake.

Jalila alisota kwenye kizuizi cha halali kwa muda wa miezi minane bila mashtaka, alikaa kwenye kifungo cha peke yake kwa muda wa miezi mitatu. Katika jaribio la pamoja la kusaidia kesi ya Jalila imepelekwama mahakamani, wanaharakati walianzisha kilio cha umoja kwenye mitandao ya Twitter na Facebook. Hatimaye alifunguliwa mashtaka rasmi, ijapokuwa mashtaka yalijumuisha msururu wa uhalifu, na pili shtaka hilo lilibeba hukumu ya kifo. Ushahidi mkuu wa mwendesha mashtaka dhidi yake ni ushuhuda wa video zake. Imejenga kesi dhidi ya Nagla, ambaye kwa sasa yuko kizuizini. Uendeshaji mzima wa



kesi ya Jalila ulikuwa kwenye mtandao wa Twitter. Mahakama ilimkuta Jalila na hatia ya kutekeleza njama za kihalifu ila ikatoa amri ya kuachiliwa kwake mara moja ikisema miezi 10 aliyokaa jela ilikuwa adhabu tosha.

Zaidi ya kampeni, intaneti pia inatumika kuchangia fedha. Mwaka 2013, Wasudan walifanikiwa kuchanga fedha katika *Kickstarter*, ambao ni mtandao wa intaneti wa kufanya michango, kutengeneza filamu *Sudan Yetu* iliyotengenezwa kuwahamasiha vijana wa Kisudan kufikiri tofauti kujihusu na kwaajili ya mstakabali wao.

Matumizi ya vyombo vya kimtandao haki-ka inaleta nafasi mpya kwa wanaharakati kusambaza taarifa na kufanya kampeni, hususan katika mazingira yakugandamizwa sana. Hata hivyo, Wasudan wanaonyesha jinsi intaneti pia inatoa nafasi kwa serikali mbaya zinapotumia vyombo hivi dhidi ya wanaharakati. Ni wazi sana kwamba serikali inajihusisha na ukaguzi katika intaneti dhidi ya wanaharakati. Idadi fulani ya waandamanaji waliozuiwa katikati ya mwaka 2010 inaripotiwa kuwa wanalazimishwa na mawakala wa Usalama wa Taifa kutoa maandishi yao ya siri za Facebook na anwani zao za barua pepe.

Itakuwa ni makosa kufikiri kwamba Sudan imekuwa nchi ya kidijitali. Sehemu nyingi nchini Sudan maandishi yaliyopigwa chapa ama hata mazungumzo ya mdomo ndiyo njia bora ya kusambaza taarifa. Hata hivyo, matumizi ya tovuti na vyombo vya kikampeni vinatoa nafasi nyingine, kuhifadhiwa na kalamu, karatasi na kipaza sauti, katika mifuko ya kuhifadhia vyombo vya habari vya kitaalamu, mabloga na wanaharakati.

Joanna Oyediran ni meneja wa Mpango wa Sudan/Sudan ya Kusini katika Jamii Wazi ya Mpango wa Afrika Mashariki (OSIEA)

**WIDANALO
MUFANYA
WANANCHI
KUWA MANIRI**

NA NATHAN ONYANGO NA GASTA KAKAIRE





UNAWEZAJE KUWAFUNZA VIJANA KUJENGA FIKRA MUHIMU NA KUJENGA UVUMILIVU KATIKA MITAZAMO TOFAUTI? UNAWEZAJE KUWAFANYA WAJADILIANE

Kila mwaka, timu mbalimbali kutoka Uganda huungana na mamia ya wanafunzi kutoka kote duniani kuhamasisha mijadala iliyoelimika kupitia mashindano ya dunia nzima yaliyoandaliwa na Chama cha Kimataifa cha Midahalo ya Elimu (IDEA). Katika matukio haya ya kufurahisha, wanafunzi hujadiliana kuhusu masuala muhimu na mara nyingi masuala tatani-shi kama vile haki za watu waliotengwa, upatikanaji wa intaneti, kusimamisha utumizi wa michezo ya video, michakato ya uchaguzi Afrika, na laana ya rasilimali ya mafuta, pamoja na mengine.

Mpango wa kuhimiza midahalo kwenye shule za Uganda ilishika kasi sana wakati Baraza la Kimataifa la Midahalo (NDC) lilipo anzishwa miaka mitatu iliyopita. Ikisaidiwa na Jamii Wazi ya Mpango Afrika Mashariki (OSIEA), NDC walipata uhakikisho kutoka kwa asasi mbalimbali za kielimu na wakaandaa mashindano ya kwanza ya kimatifa ya midahalo ambayo yalifanyika kwenye Bunge la Uganda mwaka 2010.

Ijapokuwa hapo awali midahalo ilifanyika kwenye shule za Uganda, haikufuatilia mfumo mkali na sheria hazikufuatiwa kwa makini. Vipengele muhimu vya mdahalo

kama vile jinsi ya kujitetea na kufikiria yalipuuziwa. NDC inafundisha mfumo wa Karl Popper ambao unawapa wanafunzi changamoto ya kuelewa jinsi ya kujenga fikra muhimu na kujenga uvumilivu katika mitazamo tofauti kwa kujadiliana mitazamo husika hata kama inaleta hisia zinazogawanya. Wakiwekwa katika makundi ya timu tatu, wahusika hufanya utafiti wa pande zote za suala fulani na kutambua vipengele vikuu vya utata, wakisitiza uvumilivu katika mitazamo tofauti, na kutambua umuhimu wa kufanya kazi kwa pamoja. Katika kiwango cha chuo kikuu NDC wameanzisha mfumo mzima wa bunge la Uingereza ambao hujuishia timu mbili ambazo hupendekeza hoja na mbili ambazo hupinga.

“Kabla la mfumo wa Karl Popper, tulikuwa tunacheza tu hatukuwa tunatoa hoja,” alikiri Onesmus, mwanafunzi katika shule ya sekondari ya Mbarara.

Matokeo yake, zaidi ya shule ya 300 kote nchini zimepata mafunzo katika ufundi wa Karl Popper. Zaidi ya vijana 3,000 wameshiriki katika mashindano ya midahalo kwenye ukanda huu, kambi za midahalo na mashindano ya kitaifa ya midahalo ya shule. Kupitia ushauri wa moja kwa moja, vijana 300 wamepata mafunzo katika ujuzi wa kujadiliana na wamechukuliwa kuwa majaji na wameajiriwa kama wasimamizi, watu wanaojitolea ama wafanyakazi katika sekretarieti ya NDC. NDC inasaidia kutoa mafunzo kwa walimu, wakufunzi na makocha na pia kuanzisha klabu za midahalo mashuleni na vyuoni. Usaidizi wa kiutaalamu na mafunzo pia unatolewa na NDC kwa mashirika yaendeshaayo mijadala kupitia mafunzo kwa majaji na kuhakiki. Zaidi ya vyo vikiu 20 nchini hufanya mfumo wa bunge la Uingereza.

Moja wapo thamani kuu ya NDC ni kwamba midahalo ni kwaajili ya wote

na wamefunza azimio kuu kupeleka midahalo kwa viwango vyote vya jamii. Kukiri ushiriki wa wanafunzi wa kike zaidi katika midahalo, NDC imefikia zaidi shule za akinadada, wakiwaweka wasichana wengi wadogo katika vilabu vya midahalo ya timu. Hii imeongeza ushiriki wa akinadada hadi asilimia 30. Mwaka wa 2011, wasichana kutoka katika shule ya mabanati ya Sacred Heart, Gulu walishinda kwenye mashindano ya kitaifa.

Ingawa midahalo kwa kawaida ilifanyika mijini, NDC imewafikia shule za vijijini na kuwachukua wanafunzi zaidi, wakianzisha vilabu vya midahalo, na kufanya shuguli kwa pamoja. Kutokana na haya, asilimia 60 ya wanafunzi ambao walihudhuria mashindano ya midahalo ya NDC wametoka kwenye shule za vijijini. NDC pia inashirikiana na mashirika ya kijamii kuandaa mijadala ya kijamii kuwawezesha umma kuzungumzia masuala yanayojiri na kudai uwajibikaji kutoka kwa viongozi wa mtaa. Zaidi ya vipindi 100 vya redio na TV vimeanzishwa kuandaa mijadala ya kijamii.

Ujuzi wa kujadili iliofundishwa na NDC hupatia vijana sauti. Vijana wetu wanajifunza kutizama pande zote za mitazamo, na kushiriki katika mazungumzo. Kupitia midahalo, NDC inatengeneza uzao mpya wa vijana ambao wanajiamini, wanaweza kujieleza, wana mawazo chanya na wanauwezo wa kujadiliana. Hakika, wana mawazo chanya na wanauwezo za kujadiliana. Hakika, kuna njia nyingine ya kujenga wananchi wachangamfu ambao wanaweza kudadisi pande zote za midahalo kabla ya kufanya maamuzi yaliyo na busara kuhusu masuala yenye umuhimu wa kitaifa?

Gasta Kakairi ni mkurugenzi mkuu wa Baraza la Kitaifa la Midahalo nchini Uganda na Nathan Onyango ni mkufunzi wa midahalo wakijitolea.



WAANDISHI
HABARI KATIKA
MSTARI WA MOTO

NA EMMA DAY



WAANDISHI HABARI
HODARI AFRIKA
MASHARIKI UPATA TAABU
KUBWA KUTOA HABARI ZA
UKWELI KWA WANANCHI

Dk. Stephen Ulimboka, mweyekiti wa Jumuiya ya Madaktrari Tanzania alitekwa, kupigwa vibaya, na kuachwa katika hali mbaya katikati ya mgomo wa madaktari mwaka 2012. Ingawa serikali ilikana kuhusika, utafiti uliofanywa na gazeti la uchambuzi la kila wiki la *Mwanahalisi* lilimhusisha afisa mmoja wa usalama wa taifa kama mtu pekee aliyewasiliana na Bw. Ulimboka kabla ya kupigwa kwake. Makala haya kwenye gazeti yalikuja baada ya makala mawili yaliyochapishwa yaliyomhusisha makamu mkuu wa usalama wa taifa ya kupanga kuwamaliza wale wanaoiponda serikali na mahojiano na Dk. Ulimboka kutoka kwenye kitanda chake cha hospitali ambapo alidai usalama wa taifa ulihusika na shambulizo hilo dhidi yake.

Kufuatia madai hayo makubwa, serikali ya Tanzania ingewasilisha kesi mahakamani na kumshtaki mwandishi kwa kashfa za

uongo. Cha ajabu ni kwamba serikali iliharakisha na kulifungia *Mwanahalisi* Agosti 2012. Serikali ililituhumu gazeti kwa kuchapisha makala ya uchochezi ambayo 'yalijenga na kusambaza woga kwenye jamii' na kukiuka 'viwango vya maadili.' Kifungo hicho kilisababisha mwito wa kuitizama upya sheria ya kibabe ya Magazeti ya mwaka 1976 ambayo inampa Waziri wa Habari nguvu ya kufungia ama kufutilia mbali chombo cha habari bila taarifa ya awali ama sababu yoyote.

Gazeti la *Mwanahalisi* hapo awali lilikumbwa na kifungo cha siku 90 mwaka 2008 baada ya kuanika kashfa za ufasidi ndani ya serikali na kusababisha kujiuzulu kwa Waziri Mkuu wa wakati ule. Baadae kidogo ofisi za *Mwanahalisi* zilivamiwa na mkurugenzi mkuu karibu afanywe kipofu baada ya kumwagiwa tindikali na wafanyakazi wengine kupata majeraha ya mapanga.



Kwenye nchi jirani ya Uganda, uhuru wa vyombo vya habari unadidimia zaidi wakati mazingira ya kazi kwa waandishi wa habari yankuwa hatari zaidi na nafasi inazidi kuwa finyu. Mashambulizi dhidi ya waandishi habari yanatokea bila kujali kwa sheria kulingana na takwimu kutoka kwa Mtandao wa Haki za Kibinadamu kwa Waandishi wa habari-Uganda (HRNJ-Uganda). Mwaka wa 2010, zaidi ya waandishi wa habari 58 walipitia mifumo tofauti ya mateso., mwaka 2011 (mwaka wa uchanguzi) kulikuwa na zaidi ya visa kama hivo 107, na mwaka 2012 zaidi ya visa vya kuteswa 87 viliripotiwa.

Mei 2013, serikali ya Uganda bila kujali ilifunga vyombo vya habari vya binafsi vinne kwa karibia wiki mbili, ilijumuisha redio za KFM na Dembe FM pamoja na magazeti mawili ya kila siku ya Daily Monitor na Red Pepper kufuatia kuvuja kwa nyaraka za kijeshi zilizoonyesha kwamba yeyote atakayepinga uamuzi wa mwanaye Museveni kumridhi babake anaweza kuuliwa.

HRNJ-Uganda wanakuza na kutetea haki za waandishi habari nchini Uganda, na hutoa mbinu za mshikamano na usalama kwa waandishi habari waliokuwa hatari. Mratibu wa kitaifa wa HRNJ-Uganda Geoffrey Ssebagala alizawadiwa tuzo ya Umoja wa Ulaya ya mtetezi wa Haki za Kibinadamu mwaka 2013 kwa kazi yake. Akifanya kazi kama mwandishi wa habari wa Redio Sapianta, Geoffrey alipata shinikizo baada ya shinikizo kutoka kwa serikali kutokana na ripoti zake za ufsadi, mauaji ya kiholela, na masuala ya utawala pamoja na mengine. Kufikia mwaka 2008 Geoffrey mara kwa mara alitwa mbele ili kutaja vyanzo vyake



HIVI KARIBUNI KUMEKUWA NA MCHIPUKO WA KUTUMIA SHERIA AMBAZO SIO ZA VYOMBO VYA HABARI KUSHINIKIZA WAANDISHI WA HABARI

na kujibu tuhuma za uchochezi mbele ya kitengo cha polisi cha uhalifu wa vyombo vya habari, ambapo alihojiwa na kushinikizwa kuripoti kuhusu masuala tete ya kisiasa. Mwaka huu shinikizo likaanza kuzidi na majaribio kadhaa ya watu wasiojulikana yalifanywa ili kumteka Geoffrey. Katika jaribio la tatu, Geoffrey alitupwa chini kutoka kwenye pikipiki na wavamizi, ambao walijaribu kumteka nyara wakati alipoanguka chini., ila kwa bahati nzuri Geoffrey alifanikiwa kupiga kelele ili wapiti njia waingilie kati.

Wavamizi wale walitoroka na simu yake na kompyuta yake, na mkewe akapata simu za kutishia maisha ya mumewe. Geoffrey alizamika kutorokea hadi Nairobi ambapo alifanya kazi kwa muda.

Uganda ina idadi kubwa ya sheria zinazozuia uhuru wa vyombo vya habari. Sheria dhidi ya Ugaidi inatoa adhabu ya kifo kwa mwandishi habari yeyote ambaye anapatikana akiripoti kuhusu kikundi kilichotajwa kama cha kigaidi. Sheria mpya ya Ukaguzi wa Kuteka Mawasiliano inaruhusu serikali kupata mawasiliano ya simu na kakataza mfumo wowote wa mawasiliano kama vile faksi, barua pepe na barua za kawaida. Hivi karibuni kumekuwa na mchipo wa kutumia sheria ambazo sio za vyombo vya habari kushinikiza waandishi wa habari, kwa

kutumia mashtaka ya kihalifu ya uchochezi chini ya Sheria ya Kanuni ya Adhabu, ambayo inabeba kifungo cha gerezani, ama uchochezi wa kiraia ambayo inabeba tishio la fidia kubwa. Nchini Uganda kumekuwa na visa vingi vya ukatili wa polisi dhidi ya waandishi wa habari ambao wanaripoti maandamano ama kusambaza maoni ambayo yanauliza maswali juu ya serikali., na hamna kilichofanywa kuwafungulia mashtaka wahusika. HRNJ kwasasa wamefungua zaidi ya kesi 15 wakiuliza maswali kuhusu ukiukwaji wa haki za waandishi wa habari na hatua za serikali ambazo hutishia raha ya kuwa na uhuru wa kujieleza na uhuru wa vyombo vya habari.

Katika nchi iliyopata uhuru hivi karibuni ya Sudan ya Kusini, uhuru wa vyombo vya habari pia umepata msukosuko. Bunge la Taifa la Sudan ya Kusini katika sehemu ya pili ya mwaka wake wa 2013 ilipendekeza miswaada mitatu ya vyombo vya habari; Mswada wa Mamlaka wa Vyombo vya Habari, Mswada wa Shirika la Habari la Umma na Mswada wa Haki wa Kupata Habari. Miswaada hii inangojea sahihi ya rais kabla ya kupitishwa kuwa sheria. Nchini Sudan ya Kusini kuna mistari miekundi ambayo vyombo vya habari huvuka kwa taadhari yao, hususan ikizingatiwa kuwa taasisi za utawala wa sheria ni dhaifu na maafisa wa serikali wana nguvu na huchukulia sheria mikononi mwao. Nchi ya Sudan ya Kusini ilishuka nafasi 13 kwenye Takwimu za Dunia za Vyombo vya Habari za Waandishi bila Mipaka ya mwaka 2013-hado nafasi ya 124 kati ya nchi 179 zilizo rodheshwa – kutokana na usimamizi mkali na maafisa wa usalama katika kukabiliana na waandishi wa habari, na baada ya kuuliwa kwa Isaiah Abraham, mchambuzi wa kisiasa aliyefahamika sana.

Isaiah Abraham, Msudan Kusini ni mwandishi wa makala kwenye gazeti aliuawa nje ya nyumba yake mjini Juba mwaka 2012, jambo ambalo liliaminika na wengi kuwa lilitokana na ukosoaji wake wa usimamizi mbovu wa masula ya umma na serikali. Mwaka wa 2012, kitengo cha kitaifa cha usalama kilitoa rai kwa wahariri wote wakuu wa magazeti kudhibiti taarifa zozote zinazohusika na orodha ya siri ya maofisa wa ngazi za juu wa serikali waliokuwa wanadhaniwa kuhusika na ufisadi na inaaminika waliombwa na rais kurudisha fedha ambazo walikuwa wameiba. Vyombo vingi vimejiwekea udhibiti ili kuepuka na shida na serikali, wamebakia kutangaza kinachofahamika nchini kama “habari zisizokuwa nzito,” ambazo hujumuisha matangazo ya hafla mbali mbali, matangazo na muziki. Kujidhiti huku kunakuja na kunyima wananchi taarifa muhimu, na kuvinyima vyombo vya habari haki ya kudai uwajibikaji kutoka kwa serikali.

Waandishi habari ambao wanaozungumzia haya na walio huru Afrika Mashariki wanapata hali ngumu kutokana na kuyaanika kanuni za haki ya kufahamu kwa wananchi. Wanawekwa kando na kuadhibiwa na serikali kwa kuthubutu kulinda haki za vyombo vya habari na kutetea haki ya kuripoti habari bila kushambuliwa. Hata pamoja na hatari hizi, wanaendelea kuonyesha uhodari wa hali ya juu na nguvu ya kuendelea kuripoti habari.

Emma Day ni mwanasheria wa kujitegemea wa haki za kibinadamu.







KUTAFUTA MAZUNGUUZO KUPITIA SANAA NA UTAMADUNI

NA UMRA OMAR


“NIPE UKUMBI WA KUIGIZA NA NITAKUPATIA TAIFA”

Kufuatia ushindi wa asilimia 98.8 ya kura ya maoni ya kujitenga Januari 2011, Sudan ya Kusini ilijipatia uhuru kutoka kwa Sudan Julai 9, 2011, na kumaliza miongo miwili ya vita na uharibifu. Kote nchini, kulikuwa na furaha tele wakati viongozi wa heshima kutoka kote duniani walipokuwa wakiwasili Juba kushuhudia kuzaliwa kwa taifa jipya. Katika hotuba yake ya kwanza, rais mpya wa Sudan ya Kusini Salva Kiir Mayardit aliahidi kuimarisha umoja na kupigana dhidi ya ufsadi.

Hata hivyo, udhaifu wa taifa hili jipya umeonekana tukishuhudia mlipuko wa machafuko ndani ya Sudan ya Kusini na kuendelea kwa mvutano wa mipaka baina yake na Sudan. Kuna chuki kubwa dhidi ya watu wa Sudan ya Kusini wa-

naorejea nchini kutoka ng'ambo pamoja na wahamiaji wa kiuchumi wanaotokea mataifa jirani ambao wanaonekana kama wanachukua kazi za wazawa wal-iobakia nchini wakati wote wa vita.

Kujenga utambulisho wa kitaifa na uiano ni kazi kubwa ambayo inahitaji zaidi ya tamko la uhuru. Kuna mbinu kadhaa ambazo zipo njiani za kutumia utamaduni kujenga utambulisho wa kitaifa unaokubalika na wote. Shirika la Kitamaduni la Maya linatumia maonyesho ya sanaa kama chombo cha kufundisha jamii kuhusu masuala ya utawala kama vile ufsadi na uwajibikaji. Mkurugenzi wa shirika hili, msanii Joseph Nemaya anaufuasi mkubwa wa watu kwenye maonyesho yake na nyimbo zake huzungumzia mambo ya ukweli kama vile uhumimu wa kuja pamoja na kujenga taifa bila ufsadi.





CHOMBO CHENYE NGUVU
KABISA DUNIANI NI
KAMERA



Miezi sita tu kabla ya uhuru, Kampuni ya Sanaa ya Sudan Kusini (SSTC) walifanya maonyesho yao ya kwanza katika tamsaha la dunia la Shakespeare. Taifa changa la dunia lilicheza mchezo wa Cymbeline uliotafsiriwa kwa kwa lugha ya Kiarabu cha Juba, ambayo haiandikwi. Onyesho hili iliweka wazi uwezo wa kuishi pamoja na mtu ambaye zamani hamkuweza kuishi naye na kuhitimishwa vema kwa waigizaji kuimba wimbo wa taifa wa Sudan ya Kusini.

Joseph Abuk, mmoja wa watayarishaji wa mchezo wa Cymbeline, alisisitiza umuhimu wa utamaduni katika kujenga utambulisho wa kitaifa kwa kuwajumuisha makabila yote, kukuza kujiamini na kusaidia kutambua na kueleza nani ni Msudan wa Kusini katika kipindi cha mabailiko ya kisiasa wakati ujenzi mpya wa uraia na umoja unatengenezwa. Abuk anasema, "Michezo ya kuigiza pengine ndio kishawishi kikubwa zaidi cha kufikia hisia za watu. Unaweza zungumzia suala kwa njia ya utani, watu wanaweza cheka na kudhani kwamba waigizaji hawa ni watundu tu, ila mwishowe wanaenda nyumbani na ujumbe. Ukabila sio sababu ama uhusisho wa kisiasa." Mwanzilishi mwenza Derik Uya Alfred anaongeza, "Kuna msemu wa zamani unasema-nipe ukumbi wa kuigiza na nitakupatia taifa."

Nchini Kenya, kabla ya uchaguzi wa urais Machi 2013, "Kuta za Amani za Kibera" mradi wa sanaa ya umma ulianzaishwa na vijana kusherehekea utofauti na kuhimiza umoja miongoni mwa makabila na vikundi vya kisiasa kufuatia machafuko ya kikabila wakati wa uchaguzi tata wa urais mwaka 2007. Mradi huu ulifanyika Kibera, kitongoji duni cha Nairobi ambacho kilikuwa kitovu cha mkasa wa machafuko ya 2007. Kitongoji cha Kibera kilishirikiana na msanii wa kuchora kuta wa Marekani Joel Bergner kwa warsha ya wiki sita iliyoongozwa na vijana 30 kuhusu kujenga amani. Kila mwanafunzi alipaka rangi ukuta kuoonyesha utambulisho wake. Watu walibadilishana mawazo kuhusiana na michoro hio.

Mwaka 2007, wakati wa machafuko ya baada ya uchaguzi watu wengi walitesekeka, hususan watoto. Hawakushiriki katika vita na wengi wao wakawacha bila makazi. Tumeamua kupiga rangi ukuta kwajili ya amani katika uchaguzi wa 2013. Michoro hii ni kwajili ya kujenga umoja baina yetu wakati tunapoiishi pamoja. Hatukuchagua makabila yetu ila tunaweza kuamua kuishi kama ndugu.

- Mwanafunzi wa Kitongoji cha Kibera

Wasanii wa michoro ya ukutani walichukua mfano huu kutoka kwa kuta za Kibera hadi kwenye mitaa ambayo ipo karibu ambapo treni hupitia. Shirika la Reli la Rift Valley walitoa ruhusa kwa treni zao kuchorwa na rangi kwajili ya jumbe za amani.

"Kile tunachofanya na treni hapa kwasasa ipo miongoni mwa mpango wa elimu ya uraia na njia ya kutangaza amani," anasema Uhuru B, mchoraji wa ukuta mwenye umri wa miaka 27. Mchoraji mwenza Swift9 aanaongeza na kusema: "Kwa kuwa watu hawajawahi ona kitu cha namna hii ni lazima waangalie. Na ni lazima waifikirie haya wakati wanapiga kura." Kuta za Amani za Kibera zilipata kushika hisia za vyombo vya habari vya kimataifa kama vile National Public Radio (NPR), CNN na Reuters.

Mpiga picha ambaye ametuzwa na kuheshimika Boniface Mwangi anatambulika chini ya ujumbe wa Kenya ni Kwetu na mwanzilishi wa Picha Mtaani. "Najiita mwanaharakati wa picha. Chombo chenye nguvu kabisa duniani ni kamera. Kamera imetumiwa kuwaangusha chini madikteta na kushawishi mabadiliko," anasema. Kabla ya uchaguzi wa mwaka 2013, Wakenya

waliamka na kukuta kuta zimechorwa na Mwangi akionyesha wanasiasa wa Kenya kuwa kama ndege tai, akiwahimiza wananchi wafrikie kwa makini kuhusu upigaji kura wao. "Sauti yangu, kura yangu, mustakabali wangu"ndio ilikuwa ujumbe (jambo lililomfanya Mwangi kukamatwa na polisi kujibu tuhuma za kuharibu mali ya umma). Kazi ya Boniface Mwangi inaendelea kuchochea mazungumzo katika kazi ya kisiasa, kuanzia ukiukwaji wa sheria hadi ufasidi nchini Kenya.

Katika eneo kama la Afrika Mashariki ambapo utofauti unachochea kisiasa kutenga na kubagua, kuna haja ya kujenga mazungumzo mbadala ya kuleta watu pamoja. Sanaa inaweza kuchochea wale wenye akili na hisia, na kuanzisha ulingo mzuri wa utetezi. Taarifa zinapitishwa kupitia njia zinazoweza kupatikana na za kufurahisha. Kazi za namna hii zinaendelea kota Afrika Mashariki na wasanii wenye vipaji, waigizaji, wachora katuni na wanamuziki ambao ujumbe wao wa utawala, utawala wa sheria na ujumuisho wa kijamii kwa ustadi unajumuishwa katika lingo ambazo tunaweza ungana pamoja na – sanaa, muziki, nyimbo, na michezo ya kuigiza.

Umra Omar ni mwandishi wa kujitegemea





1 2 3 4 5 6 7 8 9 0

MAKOSA KATIKA VITA DHIDI YA UGAIDI

NA EMMA DAY



**“VITA DHIDI YA UGAIDI”
INATUMIWA KUFICHA
UNYANYASAJI MBAYA
AFRIKA MASHARIKI,
KAMA VILE KUTESWA,
KUKABIDHIWA KWA
WASHUKIWA WA KIHALIFU
KUTOKA NCHI MOJA HADI
NYINGINE, KUPOTEA KWA
WAHALIFU, NA MAUAJI**

Tarehe 11 Julai, 2010, watu wa jiji la Kampala walipokusanyika kutazama mechi ya fainali ya Kombe la Dunia 2010 kwenye televisheni, watu sabini walipoteza maisha yao baada ya mlipuko ambao unaaminika ulisababishwa na kikundi cha Kisomali cha kigaidi cha Al Shabaab. Serikali za ukanda huu pamoja na zile za kimataifa walitaja shambulizo hili kama sehemu ya vita vya kimataifa “dhidi ya ugaidi” na shambulizi hili likatumika kuhalalisha miitiko ya siri na isiyo fuata sheria.

Jamii ya Wazi ya Mpango wa Haki (OSJI) waliaanda ripoti wakichambua kwa undani mwikio kuhusiana na mlipuko wa bomu kwenye Klabu ya Raga ya Kyadondo mjini Kampala iitwayo *Vita dhidi ya Ugaidi na Ukiukwaji wa Haki za Kibinadamu nchi-*

ni Kenya na Uganda: Mlipuko wakati wa Fainali wa Kombe la Dunia na Zaidi. Ripoti inatoa taarifa ya zaidi ya wanaume 12 wanaotuhumiwa kuhusika na mlipuko huo, wengi wao ni Wakenya ambao walikamatwa na kuzuiwa nchini Kenya, ikidaiwa kuwa wameteswa na maafisa wa usalama, na baadae kufurushwa hadi Uganda kisiri bila kufuata mkondo wa sheria.

Chini ya Sheria za Kenya mtuhumiwa anaweza kupelekwa nchi nyingine kufunguliwa mashtaka chini ya Sheria ya Ukabidhi wa Watuhumiwa kutoka nchi moja hadi nyingine ya mwaka 1968, ambayo inaweka utaratibu muafaka kufuatwa, pamoja na kutoa kibali cha kukamatwa, kufuatiwa na kusikilizwa mahakamani na mshukiwa anapewa uakilishi wa kisheria, kabla ya ku-

“

KUTOKANA NA DHANA NZIMA YA KULINDA USALAMA WA KITAIFA NA SERIKALI MARA NYINGI HUSABABISHA KUNYIMWA KWA HAKI ZA MSINGI ZA KUPATA TAARIFA

kabidhiwa kwa dola nyingine. Washukiwa wa Kenya kwenye mlipuko wa Kampala hawakukabidhiwa kwa dola ya Uganda, ila walijisalimisha na walikabidhiwa kisiri – kitendo ambacho majaji wa Kenya walidai ni kinyume na matakwa na katiba.

Kukabidhiwa kisiri kwa watuhumiwa ni kosa kubwa dhidi ya haki za kibinadamu kwasababu inahusisha ukadhi wa washukukiwa kutoka dola moja hadi nyingine bila uzingatiaji wa sheria. Washukiwa mara nyingi wanakamatwa kisiri, na familia zao hazipewi taarifa, hawapewi wanasheria kuwatetea madai dhidi yao, na huenda wakapelekwa kenye mataifa ambayo wanaweza kuteswa.

Ukabidhi wa kisiri ambao ulikuwa kinyume na sheria kwa washukiwa wa mlipuko kwenye ukanda huu umewacha Waislamu wengi wa Kenya na jamii ya Wasomali wahisi kama jamii zao zinalengwa na vikosi vya usalama vya Kenya, pamoja na Kitengo cha Polisi dhidi ya Ugaidi (ATPU) ambacho hufanya kazi kwa siri kubwa, na kinaamini-ka na wengi kuhusika na kupotea na kuuwawa kwa jamii zilizotengwa hivi karibuni.

Katika ripoti ya Shirika la Wakenya Kwajili ya Amani na Haki (KPTJ) wananukuliwa wak- isema kama ATPU wanahusika na ukiukwaji wa haki za kibinadamu inaanika *“dharau lao kubwa katika mchakato wa uchunguzi, mchakato wa kufungua mashtaka na mahakama”*. Mashirika ya Kiraia yanayohusika na jamii zilizotengwa nchini Kenya yanakubaliana kwamba wakati washukiwa wa ugaidi wanapoletwa mbele ya haki kupitia mahakama ya sheria, sheria ikufuatwa na ambapo kunakuheshimu kwa haki za kibinadamu, kuna heshima zaidi, uaminifu, na ushirikiano kutoka kwa jamii hizo na hii husaidia kupunguza hali ya imani kali ya dini na ukuaji wa makundi ya kigaidi.

Nchini Uganda, washukiwa wa mlipuko wa Kampala wanadai waliteswa na kutotendewa haki mikoni mwa maafisa wa usalama wa Uganda, kwa kuwekwa katika kifungo cha mwenyewe, kuchapwa, kulazimishwa kuwa uchi, kunyimwa chakula na maji, na kunyimwa uakilishi wa kisheria. Washukiwa wengi pia wanadai mawakala wa Kitengo cha Kijasusi cha Marekani cha FBI pia huwatesa na pia maafisa kutoka katika kitengo cha ujasusi cha Uingereza pia walihusika na uchunguzi.

Nchini Uganda, wasimamizi na wanasheria wanaowawakilisha washukiwa wa ugaidi pia wanachukuliwa kama wahalaifu, kama vile Al-Amin Kimathi na Mbugua Mureithi ambao walikamatwa na kuzuiwa na vikosi vya usalama vya Uganda kwasababu wanafuatilia na kutoa usaidizi wa kisheria kwa washukiwa wa mlipuko wa Kampala.

“Vita dhidi ya Ugaidi” chini ya usimamizi wa Marekani na Uingereza umetoa uhalalishaji mpya wa mipango ya siri katika msingi wa usalama wa kitaifa Afrika Mashariki na kutoa uhalalishaji wa kiwango hatari wa kutafuta taarifa kwa njia yoyote ile kwa msingi wa usalama wa kitaifa. Uhalalishaji wa kimya kimya na kufadhilwa kwa polisi na serikali za Marekani na Uingereza kwa matumizi ya kukamatwa kiholela na kukabidhiwa kwa nchi nyingine kwa washukiwa, na kuzuiliwa kwa sheria za haki ya kupata habari ambazo hugandamiza mashirika ya kiraia, inaweza kuzitenga zaidi jamii zilitengwa na kuchochea zaidi hali ya imani kali ya kidini kuliko kuimarisha usalama wa kitaifa.

Baada ya mlipuko wa Kampala serikali ya Uganda ilipitisha Sheria ya Ukaguzi wa Kuteka Mawasiliano ambayo inaruhusu serikali kupata mawasiliano ya simu na kakatiza mfumo wowote wa mawasiliano kama vile simu, barua pepe na faksi. Mashirika ya kiraia wanahofia kwamba serikali ya Museveni inatumia woga wa wananchi kuhusu ugaidi kufunika sheria za kibabe ambazo hugandamiza yoyote anayepinga serikali pamoja na mashirika ya kiraia na wanasheria wa haki za kibinadamu.

Kutokana na dhana nzima ya kulinda usalama wa kitaifa na serikali mara nyingi husababisha kunyimwa kwa haki za msingi za kupata taarifa, OSJI wamekuwa wakiandaa kanuni mbali mbali, Kanuni za Kitaifa za Usalama na Haki ya Kupata Taarifa, ambayo inapendekeza miongozo ya nja ambazo serikali zinaweza kutumia kisingizio cha kulinda usalama wa kitaifa, wakidhamiria kusaidia wananchi kupata taarifa kuhusu usalama wa kitaifa duniani kote.

Mnamo Mei, 2012, Jamii Wazi ya Mpango wa Afrika Mashariki (OSIEA) pamoja na OSJI walishirikiana na kuitisha mkutano wa siku mbili katika ukanda wa Afrika Mashariki kujadiliana kuhusu kanuni hizi, kwa lengo la kupata mtazamo kutoka kwa mashirika ya kiraia, serikali katika ukanda huu ilikufahamu jinsi gani kanuni hizi zinaweza jumuishwa katika miktadha wa kisheria na kisiasa ya Afrika Mashariki. Kulikuwa na majadiliana changamfu kutoka kwa mawaziri kutoka Sudan ya Kusini, Sudan, Kenya, Uganda, Rwanda, Uhabeshi na Tanzania, pamoja pia kutoka kwa mashirika mbali mbali ya kiraia, wanasheria na wawakilishi wa polisi kutoka kwenye ukanda huu. Mapendekezo yaliyotoka kwa washiriki yalichukuliwa na OSJI ili kujumuishwa kwenye toleo la mwisho.

Sababu za kulinda usalama wa kitaifa ambazo nia za ukweli na zilizoainishwa vema ni sababu kuu za serikali kuzuia taarifa fulani. Hata hivyo, hii lazima ipimwe na ile haja a ushiriki wa wazi na kufutaliwa kwa ukaribu kwa serikali kupitia upatikanaji wa taarifa kwa umma. Viwango pana na visivyoeleweka vya usalama wa kitaifa vinautoa fursa ya kufichwa kwa masualaharamu na kuzuia uwezo wa watu kupata haki.

Tangia mwaka 2001, wakati “vita dhidi ya ugaidi” ilipoanza, usalama wa kitaifa umeutumika kuficha ukiukwaji wa haki za kibinadamu kama vile kuteswa, kupotea, na mauaji. Taarifa hizi zinapaswa kuwa wazi kwa wananchi. Kanuni za Kitaifa za Kitaifa za Usalama na Haki ya Kupata Taarifa zinatoa mfumo mzuri wa kuongoza serikali wakati wanapotaka kutumia usalama wa kitaifa kuzuia upatikanaji wa taarifa.

Emma Day ni mwanasheria wa kujitegemea wa haki za kibinadamu.



WAUZA NGONO

KATIKA MSTARI

WA MBELE WA

KUTUMIA UJUMBE

MFUPI (SMS)

NA HEATHER DOYLE NA RACHEL THOMAS

“

KWA JAMII AMBAYO KWA MUDA MREFU IMETENGWA NA KUNYANYAPALIWA, TEKNOLOJIA YA SIMU ZA MKONONI (RUNUNU) IPO MSTARI WA MBELE KUWASAIKIA WAUZA NGONO KUDAI HAKI ZAO NCHINI KENYA

Wauza ngono mijini na katika majiji makubwa kote nchini Kenya wanaripoti viwango vikubwa vya dhuluma ya kimapenzi pamoja na kuteswa kimwili, na mateso mengine yanayokiuka haki, hususan kutoka kwa polisi na maofisa wengine wa usalama. Dhuluma hizi huongeza uwezo wa kupata maambukizo ya Virusi vya Ukimwi (VUU) pamoja na hatari zingine za kiafya. Katika mwaka wa 2003, ilikadiriwa kuwa asilimia 75 ya wauza ngono mjini Kisumu, Kenya, walikuwa wameathirika na VUU. Shirika la Keeping Alive Societies' Hope (KASH) linalofanya kazi magharibi mwa Kenya, walitambua kwa haraka kwamba viwango vya juu vya madhila ya polisi na ukosefu wa mipango ya kudhitibi haya madhila ilimaanisha kuwa kampeni za kawaida za kuhimiza watu watumie mipira ya kondumu na mafunzo ya kiafya ya kuinga maambukizi ya VUU miongoni mwa wauza ngono hayatoshelizi.



**MAJIBU YA HARAKA
KUPITIA UJUMBE MFUPI
WA SIMU UMESAIDIA
KATIKA KUPUNGUA KWA
HARAKA KWA DHULUMA
DHIDI YA WAUZA NGONO**

Jinsi ya kuwasaidia wauza ngono ambao wanakumbwa na matatizo ya dhuluma ama kukamatwa na polisi ndio cha muhimu katika kuokoa maisha na kulinda usalama wa mtu. Kwa kutambua hili, KASH walianzisha mfumo wa dharura wa simu za mkononi uitwao “Ujumbe Mfupi Mbele”. Mfumo huu unawaunganisha wauza ngono wa Kisumu na wasaidizi wa sheria pamoja na vikundi vingine vya watu ambavyo vinaweza kutoa usaidizi wa haraka. Majibu ya haraka kupitia ujumbe mfupi wa simu umesaidia katika kupungua kwa haraka kwa dhuluma dhidi ya wauza ngono.

KASH pia wamejenga mazungumzo bora pamoja na polisi. KASH wanashirikiana pamoja na Idara ya Polisi ya Mkoa wa Nyanza magharibi mwa Kenya kuwafundisha maafisa wa polisi mara moja kila baada ya miezi mitatu kuhusu haki za wauza ngono. Zaidi ya maafisa 600 wamepata mafunzo. Kupitia mpango huu, wauza ngono 10 na maafisa polisi 10 walifundishwa kuwa wakufunzi baina yao na kuanzishwa kwa mfumo wa kukusanya taarifa za dhulu-

ma. Hii imekuza uhusiano mwema baina na wauza ngono na polisi. KASH pia wanawafundisha wauza ngono kuwa wasaidizi wa sheria ili wawe na ujuzi mwingi katika masuala ya haki za kibinadamu na sheria za kitaifa ili kulinda wauza ngono wenzao wanaopitia dhuluma ama wanaotafuta msaada wa kisheria katika masuala kama kuomba dhamana wanapokamatwa.

Wakishirikiana, wasaidizi wa sheria na polisi wanaotoa mafundisho walianzisha mfumo wa “Ujumbe Mfupi Mbele” kripoti na kufuatilia dhuluma za haki za kibinadamu, kutuma taarifa muhimu za haki za kibinadamu na kujenga mitandao ya watu wanaojihusisha na kazi za KASH. KASH hutuma ujumbe mfupi kila wiki kwa mtandao wa wauza ngono. Ujumbe unakuwa wa maelezo, ukiazimia kuelewa dhuluma dhidi ya haki za kibinadamu ambazo hufanyika, na za kujuza, wakiwajua kuhusu taarifa mpya za haki za kibinadamu. Ili kuongeza maoni ya mauza ngono, majibu huwa ya ndio au hapana, na ujumbe unahamasisha wanaojibu kuwapigia na kuelezea maoni yao kwa mazungumzo. KASH wanapata kama majibu matano kwa kila ujumbe. Pia, wauza ngono hupewa mafunzo ya jinsi ya kutuma ujumbe mfupi kwa KASH ama wasaidizi wa sheria kuwashtua kama kuna dhuluma zozote zinatokea na kama wanahitaji msaada wa kisheria. Mtandao wa wasaidizi wa kisheria kisha wanawahamasisha kujibu kwa kwenda hadi sehemu dhuluma, kuwahabarisha marafiki katika eneo, ama kujitokeza kwenye kituo cha polisi.

Mfumo huu umefanikiwa kutatua kesi mbali mbali za dhuluma. Katika mfano mmoja, muuza ngono mmoja ambaye alipata ujumbe mara kwa mara kutoka kwa KASH alipiga simu kuripoti afisa wa polisi ambaye alikuwa anachapa na kuwasumbua wauza ngono usiku. KASH walijibu kwa kumkaribisha msimamizi wa afisa yule katika moja wapo ya hafla za kila mwezi na kujibu na kuripoti kile kisanga. Afisa yule alikemewa, na wauza ngono katika eneo lile wakaripti kuwa tabia yake kwa wauza ngono ikaimarika sana. Mfumo huu pia umefanikiwa katika kuwashirikisha wauza ngono katika mpango wa utetezi na huduma wa KASH. Mmoja wa wauza ngono ambaye alipata ujumbe mfupi wa mara kwa mara alimwambia rafiki yake kuhusu kazi na huduma za KASH na kumshauri audhuri warsha ya elimu ya afya iliyokuwa ikifanyika hio wiki. Rafiki yule aliudhuri warsha ile, na akashauriwa kupata matibabu ya maambukizo ya zinaa ambayo yalikuwa yanamsumbua. Hivi karibuni, KASH walitumia Ujumbe Mfupi Mbele kuwahamasisha wauza ngono pamoja na wanajamii kutimiza wajibu wao kama wananchi kupiga kura.

Mfumo wa ujumbe mfupi unawapa fursa KASH kupata maoni ya mara kwa mara kutoka kwa wauza ngono kuhusu maisha yao na kuandaa mipango yao ya utetezi ili kuambatana na mahitaji yao. Maoni haya kutoka kwa ujumbe wa SMS mara kwa mara hukisanywa na kuchambu-

liwa ili kuweka msingi wa hafla za utetezi ambazo zinaudhuriwa na maofisa wa polisi, wauza ngono, wanasheria pamoja na wafanyakazi wa KASH. Mfumo wa Ujumbe Mfupi Mbele pia umekuwa kichecheo cha kujenga ushirikiano baina ya vikundi vinavyofanya kazi kulinda haki za wauza ngono nchini Kenya. Wazo hili limewafikia – muungano wa kuwahamasisha wahudumu wa baa (BHESP) pamoja na washirika wao kisheria wa Kituo cha Haki ya Elimu na Ufahamu (CREAW) watekeleza mpango kama huu uitwao jukwaa la HUDUMA jijini Nairobi.

Matumizi ya ujumbe mfupi wa simu umesaidia katika upunguaji wa dhuluma za haki za wauza ngono. Teknolojia ya rununu imekuwa njia ya wauza ngono wa Kenya kubadilisha maisha yao na kudai haki zao.

Heather Doyle ni mshauri wa Shirika la Jamii Wazi ya Mpango wa Afya ya Umma na Rachel Thomas ni afisa wa juu wa Mpango wa Afya ya Umma.



Exit poll distorts Kenyan election

How an exit poll by the
Kenya's official media
presidential election
incumbent President Mwai Kibaki
and opposition leader Uhuru Kenyatta

Official results

Kibaki 46%
Other <1%
Musyoka* 9%
Odinga 44%

Not exit poll

Odinga 46%
Musyoka* 10%
Other 4%
Kibaki 40%

Kalenjin
Kalenjin

gate
e to rounding

UGANDA

100 km
100 miles

KENYA

★ Nairobi

UNITED
REP. OF
TANZANIA

Total votes cast on Dec 27 **9.9 million**

Source: Exit poll of 5,495 voters from all eight Kenyan provinces (69 out of 71 districts, 179 out of 210 electoral constituencies) by Clark C. Gibson and James D. Long, Department of Political Science, University of California, San Diego. Margin of error: +/- 1.32 percentage points. Poll funded by the International Republican Institute, McClatchy Washington Bureau, ESRI. Graphic: Melina Yingling, Judy Treble

HABARI



MWITO WA KIMYA WA UWAJIBIKAJI HABARI VANDISHI HABARI

NA DAVID MAKALI



**JE, AMANI KWA NJIA
YOYOTE ILE INAMAANISHA
UKIMYA KUTOKA KWA
VYOMBO VYA HABARI?**

Maoni yaliyochapishwa kwenye jarida la International Herald Tribune Machi 13, 2013 na mwandishi wa habari wa Kiingereza Michela Wrong yanatoa picha halisi ya hali ya udhaifu wa uandishi habari nchini Kenya katika miaka ya hivi karibuni: “Kwa mara kadhaa utahisi kama jeshi la mazimwi limeteka na kuchukua nafasi ya zamani ya sekta changamfu ya uandishi habari ya Kenya, huku waandishi wa habari wa Kenya wakizubaa.” Mfuatiliaji wa siku nyingi wa sekta ya habari na siasa za Kenya, Wrong anachanganua waandishi habari wa Kenya waliobaki

kuwa watazamaji wakati wa uchaguzi mkuu wa Machi 2013 ambao ulikuwa wenyewe ushindani mkubwa sana, uchaguzi wa kwanza baada ya ule wa mwaka 2007 ambao ulikumbwa na machafuko.

Sekta ya uandishi wa habari Kenya ambayo inasifika kama bora zaidi Afrika Mashariki – na kote katika bara la Afrika – sekta ya uandishi wa habari nchini Kenya imepata changamoto kubwa katika suala la kuaminika kwa wakati huo huo ikisifiwa na maofisa wa serikali pamoja na wanasiasa kwa uwajibikaji na uzalendo.



UWAJIBIKAJI KATIKA UANDISHI
HABARI KATIKA MUKTADHA WA
KENYA SASA UNAMAANISHA
KUFICHA MAMBO FULANI

Sifa hizi hazistahili kulingana na wahakiki: “Mwandishi wa habari yoyote ambaye ana hadhi lazima ajishuku pale anapopata sifa kutoka kwa wale walio madarakani,” anasema Wrong, akitoa mfano wa jinsi uchaguzi mkuu wa 2013 ulivyoripotiwa. “Vyombo vya habari lazima wajiulize kama, katika uchu wao wa kuripoti vema, walikubali dhuluma nyingine kubwa kutokea mbele ya macho yetu.”

Wakati serikali na vikundi vya amani vikivipa vyombo vya habari sifa kedekede kwa kampeni zao za amani kama uwajibikaji katika uandishi habari, wahakiki wanapuuzia haya kama kupuuzia kazi yao muhimu. Kulikuwa na “ukosefu mkubwa katika maadili ya kikazi,” anasema mwandishi wa habari wa siku nyingi John Gashie akivilaumu vyombo vya habari kwa “kuwa bubu” wakati wa uchaguzi.

Kuelekea uchaguzi wa 2013, hapakuwa na uchambuzi wa kina kuhusu watu binafsi waliokuwa wana kesi mbele ya Mahakama ya Kimataifa ya Uhalifu (ICC) kwa makosa ya uhalifu dhidi ya binadamu kama wanasapaswa kugombea nyadhfa huku uchambuzi wa namna hii ukipondwa kwa madai ya ukoloni mambo leo ama kuingiliwa kisiasa. Baada ya uchaguzi, madai ya wizi wa kura yalizimwa kwa haraka. Mwanablogu mmoja Patrick Gathara kwa ufasaha alitaja hii kama “upasuaji wa amani,” akisema:

Mshikamano mzuri ulizuka baina ya vyombo vya habari na umma. Kenya ingekuwa na uchaguzi wa amani na haki bila shaka. Mjadala uliendeshwa na sauti fulani za kipekee na pasingekua na vipingamizi...wacha walio lala walale, hio ndio ilikuwa kauli mbiu ya kitaifa...nani anajali kuhusu udhabiti wa matokeo ya uchaguzi? Kuna shida gani kama baadhi ya kura hazikuhesabika? Tulikuwa na amani...sahau hayo, usiulize maswali, usihoji. Kubali na uondo.

Uwajibikaji katika uandishi habari katika muktadha wa Kenya sasa unamaanisha kuficha mambo fulani. Vyombo vya habari vimepatwa na woga katika kuripoti chochote ambacho kitazua taharuki ama kufuma machafuko, baada ya kuanika wizi wa kura katika uchaguzi wa mwaka 2007 na machafuko yaliyotokana na uchaguzi. Kutokubali kukiri makosa haya ni mbaya sana – vyombo vya habari vilikataa kata kata kuchochochea chuki za kikabila hata baada ya Joshua arap Sang, mwandishi wa habari wa redio, kukumbwa na mashtaka ya makosa ya uhalifu dhidi ya binadamu kwenye mahakama ya ICC.

Kutokana na madai haya, wakati wa uchaguzi wa 2013, vyombo vya habari kwa mshikamano waliripoti msimamo rasmi na kutupilia mbali malalamiko yaliyoletwa

mbele na washindani wa kisiasa. Huku haya yakisifiwa na serikali, wachambuzi waliwashtumu vyombo vya habari kwa kuendekeza ukiukwaji wa haki muhimu. Hata na ukimya wa vyombo vya habari, mitazamo ya nguvu ya chuki na taharuki za kikabila bado imebaki, ikikitokeza sana sana kwenye Facebook na mitandao mingine ya kijamii.

Dawa ya kuwa na uwajibikaji katika sekta ya uandishi habari ipo ndani ya uandishi habari yenyewe. Kama daktari kwa mgonjwa, mwandishi wa habari mzuri lazima awe makani kuhakikisha taarifa anazozitoa zitawafaidi wananchi na hazitawadhuru. Hata hivyo haya hayazingatiwi nchini Kenya ambapo vyombo vya habari ni vinasahau uwajibikaji kwa wananchi na kuangalia zaidi faida ili kujikimu.

Uwajibikaji katika uandishi habari unabaki kuwa mwito katika wakati huu wa intaneti.

David Makali ni mkurugenzi wa Taasisi ya Vyombo vya Habari (The Media Institute) na ni mchambuzi wa masuala ya kisiasa



KUTOKA VYOMBO VYA HABARI VYA KITAIFA HADI UHURU KATIKA UTANGAZAJI

NA JEGGAN GREY-JOHNSON



**VIKONEKANA KAMA
MSEMI WA SERIKALI,
VYOMBO VYA HABARI
VYA KITAIFA VIMEPOTEZA
UAMINIFU NA UMAARUFU**

Wakati mji wa Addis Ababa ulipokuwa mwenyeji wa sherehe za maadhimisho ya miaka 50 ya Umoja wa Afrika kulikuwa na furaha, bashasha pamoja na mapambo ya risala za kujipongeza; viongozi wakizungumza baina yao. Mashirika ya kiraia yalizuilwa katika sherehe hizo. Ungedhani kwamba mataifa ya Umoja wa Afrika yalikuwa yametimiza malengo yao yote. Kwa hakika mafanikio ni kidogo, ukiondoa mikataba 43 ya kikanda, ukianzia na Mkataba wa Umoja wa Muungano wa Afrika wa Mei mwaka 1963 hadi wa hivi karibuni – Mkataba wa Maadili na Kanuni za Huduma ya Umma na Utawala. Mengine ni Mpango wa Afrika Kujitathmini Kiutawala Bora (APRM), Mkataba wa Demokrasia, Bunge la Umoja wa Afrika, Mahakama ya Afrika, na Ushirikiano Mpya wa Maendeleo ya Afrika. Ila kanuni za mikataba hii na taasisi hizi za utawala kwa kiasi kikubwa zimekosa ufanisi; hazifuatwi na zinadunishwa na kuharibiwa na viongozi wale waliokubali kuvianzisha.

Maendeleo katika teknolojia ya vyombo vya habari yameimarisha ufahamu, ubora, uchaguzi na upatikanaji rahisi kwa taasisi na mikataba hii kwa kiwango cha juu katika miaka ya hivi karibuni. Mataifa ya Afrika yamesisitiza wajibu wao kuheshimu kanuni kuu za uhuru wa kujieleza. Nchi nyingi zimepitisha sheria za kimataifa na kuwa sheria nchini mwao pamoja na sera zinazohamasisha uhuru wa maoni

na haki ya kutafuta, kupata na kutoa mawazo na taarifa kupitia mifumo waipendayo. Katika ngazi ya kikanda, kuna Azimio la Windhoek la Kukuza Vyombo vya Habari vilivyo huru na Tulivu Afrika; Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu, ambao unajumuisha haki ya kupata taarifa; na Mkataba wa Afrika wa Vyombo vya Habari, na Mkataba wa Demokrasia. Hata hivyo, ni nchi chache wanachama wa Umoja wa Afrika waliokubali kutekeleza waliyoko katika mikataba hii.

Tafti zilizofanywa na Mpango wa Afrika wa Utawala na Ufuatiliaji (AfrIMAP) zinaonyesha mtindo wa ukandamizwaji wa vyombo vya habari barani Afrika kupitia utamaduni wa usiri uliomo ndani ya sheria zinazozimiza kuzinyamazisha vyombo huru vya habari na kuwatisha wale wanaoyaweka hadharani maovu yanayotendeka. Hii ni kipingamizi kikubwa cha kuimarisha maadili na kidemokrasia na utawala bora barani Afrika. Hii inakiuka haki maalum za wananchi kudai uwajibikaji kutoka kwa serikali yao. Marekebisho ya sheria hizo ni muhimu sana ili kuhakikisha uwazi na uwajibikaji katika utawala.

Marekebisho ya sheria za vyombo vya habari ni muhimu sana katika kuvigeuza vyombo vya habari vya serikali kuwa vyombo vya habari vya umma vilivyohuru barani Afrika. Kuna nchi moja tu barani Afrika ambayo inaweza dai kuwa na chombo cha habari bora cha umma, Afrika Kusini. Kwenye nchi nyingine, vyombo vya habari vinasimamiwa na bodi zinazojumuisha hususan wateule wa serikali. Makubaliano ya kazi na mfumo wa uendeshaji unafanana kwa karibu na ule wa utumishi wa umma, na serikali nyingi huendelea kuwa wasimamizi kwa wakati huo huo wakipunguza ufadhali ama kusimamisha moja kwa moja. Vikionekana kama msemi wa serikali, vyombo vya habari vya kitaifa vimepoteza uaminifu na umaarufu. Vinashindwa kuvutia vipato kutoka kwa matangazo na ufadhili.

Kuna haja ya kuunda sheria mpya ili kuhibiti sekta ya vyombo vya habari pamoja na vyombo vya habari vya serikali:

Udhibiti katika sekta ya vyombo vya habari lazima uondolewe kutoka kwa usimamizi wa serikali. Mdhibiti wa uhuru wa vyombo vya habari lazima asiwe na maslahi yoyote ya kisiasa, kibiashara, na mengine yoyote.

- Vyombo vya habari vya umma lazima visimamiwe na bodi ambayo ni huru kutoka kwa maslahi ya kisiasa, kibiashara na mengine yoyote, na viweze kulinda shirika dhidi ya ushawishi mbaya kutoka nje.

- Ufadhili lazima uwe mchanganyiko wa matumizi ya bunge, ada ya leseni na mapato kutoka kwa matangazo.

- Baraza la Mawaziri lazima liache kuiingilia bodi ya wakurugenzi ya vyombo vya habari vya umma na kuwaachia juukumu hilo bunge.

- Vyombo vya udhibiti vya mawasiliano lazima viwe huru kutoka kwa usimamizi wa serikali na uteuzi wa bodi ufanywe katika njia ya uwazi na katika uangalizi wa bunge.

Maadhimisho ya miaka 50 ya Umoja wa Afrika yamepita. Hotuba zimetolewa. Na ujumbe umepotea katika tafsiri ama kupitwa na watu bilioni moja ambao wanaishi barani Afrika. Viongozi wanapaswa kutambua kwamba baada ya miaka 50 yakuzungumza baina yao sasa ni wakati wa kuwasikiliza wananchi wao. Ni wakati wa kufanya mageuzi katika mifumo ya sheria ya vyombo vya habari na kugeuza vyombo vya habari vya serikali vya Afrika kuwa vyombo vya habari vilivyo huru kwaajili ya mstakabali wa bara hili zuri ambalo uwezo wake bado hujatumika kabisa.

Jeggan Grey-Johnson ni afisa wa mawasiliano na utetezi katika Mpango wa Afrika wa Utawala na Ufuatiliaji (AfrIMAP)

AFRIKA INA HAKI YA

KUJUA

NA MAXWELL KADIRI





**HEBU FIKIRIA BARA
LA AFRIKA AMBALO
SERIKALI ZIMEPITISHA
SHERIA MUHIMU AMBAZO
ZINAWAPA FURSA WATU
KUPATA TAARIFA AMBAZO
ZIKO KATIKA UHIFADHI WA
TAASISI ZA UMMA. TUME
YA AFRIKA YA HAKI ZA
BINADAMU INAJITAHIDI
KUTIMIZA HILI.**

Wakati wa hafla ya 42 ya Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu (ACHPR) iliyofanyika Congo, Brazaville, mwakilishi maalum wa tume hii wa uhuru wa kujieleza, Mwanasheria Pansy Tlakula alipendekeza azimio la kupanua wigo la kazi yake kujumuisha haki ya kupata taarifa barani Afrika. Azimio hili lilipita bila kupingwa.

Mwanasheria Tlakula aliaandaa vipaumbele kadhaa kwaajili ya mamlaka mapya yaliyopanuliwa, ambavyo vilijumuisha kuimarisha mipango ya kitaifa na kikanda itayodhamiria kudumisha viwango vya juu vya haki hii katika bara la Afrika, chini ya matakwa ya Ibara ya 9 ya Mkataba wa Afrika na Sehemu ya 4 ya Azimio la Tume ya Afrika ya Kanuni za Uhuru wa Kujieleza Afrika. Vipaumbele vilijumuisha kuaandaa mfano wa Sheria ya Uhuru wa Taarifa (FOI) Afrika kama kielelezo cha mataifa kuanza, kukubali, na kutekeleza sheria za upatikanaji wa taarifa katika ngazi ya kitaifa.

Kipaumbele cha pili kilikuwa utetezi wa upitishwaji na kuwa sheria kwa Mkataba wa Demokrasia, Uchaguzi na Utawala wa Umoja wa Afrika kuhimiza uwazi na uwajibikaji katika utawala Afrika chini ya maadili mema ya demokrasia. Mkataba wa Demokrasia unaeleza katika kifungu kimoja kwamba mataifa wanachama “wajitolee katika uanzilishaji wa njia muafaka za kukuza ushiriki wa wananchi, uwazi, upatikanaji wa taarifa, uhuru wa vyombo vya habari na uwajibikaji katika uendeshaji wa masuala ya umma.”

Kwa ushirikiano na Kituo cha Haki za Binadamu katika Chuo Kikuu cha Pretoria, mwakilishi maalum, pamoja na washikadau wengine, walihudhuria msururu wa makongamano ya kitaalamu kuandaa sheria mfano (model law). Baada ya miezi sita, rasimu ya sheria mfano iliwasilishwa kwaajili ya utathmini mbele ya umma na mapendekezo kwenye Hafla ya Kawaida 49 ya Tume ya Afrika mjini Banjul, Gambia. Vikundi vya kikanda vilifanya mashauriano kuhusu sheria mfano hio. Kampeni ya utetezi ilifanywa kuhimiza mataifa watie sahihi Mkataba wa Demokrasia, Uchaguzi na Utawala na kuifanya sheria; matokeo yake ilikuwa mataifa 15 wanachama wa Umoja wa Afrika walitia sahihi na kuifanya sheria mkataba huu ambao ulianza kutumia Februari 15, 2012 huku Sheria Mfano (Model Law) ya Upatikanaji wa Taarifa Afrika ulikubaliwa na Tume ya Afrika mwaka mmoja baadae Februari, 2013. Kukubaliwa na kuzinduliwa kwa sheria mfano (model law) katika Hafla ya Kawaida ya 53 ya Tume ya Afrika mjini Banjul, Gambia, mnamo Aprili 12, 2013 ilikuwa hatua kubwa katika kazi ya tume hii.


Moja wapo ya kipengele muhimu cha sheria mfano (model law) ni kwamba inapanua wigo la haki ya kupata taarifa zaidi ya taasisi za umma na kujumuisha taasisi binafsi ambazo hutumia fedha za umma, ambazo hutoa huduma za umma ama hufanya kazi za umma; ama pale taarifa hizi

huitajika katika kulinda haki za binadamu. Sheria mfano inalazimu utoaji hadharani wa vitengo vya taarifa; inatoa muda wa kujibu maombi ya taarifa; na hutoa mfumo wa upatikanaji wa taarifa ili kuhakikisha ufanisi na utatuzi wa haraka wa migogoro ya uhuru wa kupata taarifa.

Ufuatiliaji, kukubalika na usaidizi wa mchakato huu wa kuandaa sheria mfano (model law) imedhihirisha ndani na nje ya bara ufanisi wa kazi ya Tume ya Afrika. Hatua ifuatayo ni kujikita katika utekelezaji wa mkataba huu na sheria mfano (model law) ilikuhakikisha kwamba haki ya kujua kwa umma inaimarishwa barani Afrika.

Maxwell Kadiri ni afisa wa sheria wa Mpan-go wa Jamii Wazi wa Haki





KUONDOA DHANA POTOVU YA VYOMBO VYA HABARI

NA JACOB J AKOL

Katika moja wapo ya safari zangu kwa ndege kutoka Juba kuelekea Nairobi, mwanamke mzee aliyekaa kando yangu akaomba msaada, “Ninashida ya kuandika. Unaweza nisaidia kupita idara ya uhamiaji tutakapofika Nairobi?”

“Bila shaka” Nilimjibu. “Una pasipoti?”

Alisema ndio, akageukia simu yake, na kumhakikishia mtu aliyekuwa akizungumza naye kwenye simu kwamba amepata mtu ambaye angemsaidia. Bila shaka alikuwa mmoja kati ya mamilioni ya Wasudan wa Kusini ambao mradi wa Gurtong wa amani na chombo cha habari, ambao umekuwa ukibuni njia muafaka za mawasiliano. Kwa idadi kubwa wao ndio wengi.

Katika muda mfupi wa mzunguko wa haraka, na kulingana na Darwin, human evolution ilitokea sehemu fulani kwenye bara la Afrika, wakaanzisha lugha, wakazaana na kutawanyika kote duniani. Karne nyingi za kutengwa kijiografia na utofauti wa mazingira ulichanganya

na kuzalisha lugha tofauti, utamaduni tofauti na hata rangi tofauti. Sayansi na teknolojia ya kisasa na mawasiliano ya haraka, binadamu wanapaswa kujua asili yao na kwasasa wanaishi katika “kijiji cha dunia”, kulingana na Marshall McLuhan; je ni kweli? Tunaelewana kweli kama tungekuwa tunaishi kwenye kijiji? Haku na uhakika kwa hili.

Alipoambiwa kwamba Uingereza ilikuwa imeweka milingoti ya telegrafu kote hadi India, Mwingereza mmoja hakufurahishwa. “Ni kipi Uingereza na India wataambiana kwa gharama kubwa hivi?” Swali lilikuwa limewekwa vizuri, likimaanisha kwamba milingoti na nyaya zilikuwa tu njia za mawasiliano na zilifanya kazi kama nyenzo za kufikisha mawasiliano.

Ila, McLuhan, akiandika katika miaka ya 1960, angejibu tu kwa kusema: “Nyenzo ndio ujumbe,” akimaanisha kwamba nguzo zile na nyanya zilizounganishwa ndio zilikuwa ujumbe. Uelewa huu ungemeanisha kwamba vyombo vya mawasiliano kama vile mdomo, pembe, ngoma, moshi, nyaraka zilizochapishwa

“

VYOMBO VYA HABARI NI NJIA ZA MAWASILIANO NA LAZIMA ZIBUNI UJUMBE WAO KWA NAMNA AMBAYO NJIA HAITADHURU UJUMBE WENYEWE.



VYOMBO VYA HABARI
NI JUKWAA LA KILA MTU
KUTUMIA NA LAZIMA VIWE
VYA AINA NYINGI NA HURU
KISHERIA

na sauti, ambazo binadamu wametumia katika nyakati tofauti za historia kuandaa na kuwasilisha ujumbe, zilikuwa nazo ni ujumbe, ambazo hazikuhitaji uelezi zaidi ama utafsiri zaidi. Hili lina utata.

Chombo chochote kipya cha mawasiliano, kiwe chombo cha habari cha kuchapisha, telegrafu, redio, faksi, televisheni, tarakilishi ama simu za kisasa za mkononi, inasimika utamaduni wake kwa watumiaji bila kujua na kwa jamii nzima kwa ujumla. Tazama tu jinsi simu za mkononi zilivyoweza kuteka matajiri na maskini, vijana na wazee, waliosoma na wale ambao hawajasoma kote duniani, hususan kwa maskini na wale wengi ambao hawajasoma kama nchini Sudan ya Kusini! Hebu tazama vikundi vya Wasudan wa Kusini katika mgahawa ama kokote mjini Juba na utakubali kwamba hawawezi kutengana na simu zao za mkononi, labda tu kama mitandao imegoma kama ifanyavyo mara nyingi. Ila hii inavipa vyombo vya mawasiliano nguvu za ajabu na kuteka bure hisia zetu.

Wale wanaowasilisha ujumbe, hususan waandishi wa habari, lazima wakumbuke kwamba vyombo vya habari ni vyombo vya mawasiliano tu na lazima zibuni ujumbe wao kwa namna ambayo haitadhuru ujumbe wenyewe. Kutumia nyenzo mahususi kulenga wasikilizaji inabaki kuwa njia muafaka ya mawasiliano. Zaidi ya yote, vyombo vya habari ni jukwaa la kila mtu kutumia na lazima viwe vya aina nyingi na huru kisheria.

Nchi ya Sudan ya Kusini ipo katika njia panda katika sekta ya vyombo vya habari kwasasa. Wakati Gurtong Trust ilipoanzisha tovuti mwaka 2002-2003, ililenga vijana wa Sudan ya Kusini waliokuwa wakiishi ng'ambo ambao walikuwa wamezongwa na msongo wa mawazo kutokana na vita vya muda mrefu na mgawanyiko wa kikabila nchini kwao. Lengo lilikuwa nikuwapa taarifa zilizofanyiwa utafiti kuhusu makabila yao huko nyumbani na ulingo ambao ungewasaidia kuwapata marafiki zao waliopotea na ndugu waliotawanyika kote duniani, na pia kubadilishana maoni kwa ustaarabu. Hata kama kupatana kule haukuwa wa kirafiki kila mara, bado kulikuwa na mafanikio makubwa, kwani wengi wao wamekua na kusonga mbele na tovuti ya www.gurtong.net.

Gurtong imeandaa mamia ya vipindi vya redio vilivyoandaliwa kwa msingi wao wa malengo ya umoja katika utofauti na kusherehekea maadili endelevu ya tamaduni tofauti nchini Sudan ya Kusini. Vituo kadhaa katika maeneo mengi ya Sudan ya Kusini vinarusha vipindi hivi.

Ili kuchangia katika mchakato wa amani kwenye jimbo la Jonglei, ambapo makabila matatu kati ya sita yamekuwa yaki-pigana baina yao, Gurtong walianzisha "Mpango Dijitali" kwa lengo la kurekodi jumbe za amani na mipango ya kukuza amani miongoni mwa makabila. Kisha jumbe hizi zinatafsiriwa kwa lugha nyingine mbili; hivyo jumbe katika lugha ya Murle hutafsiriwa kwa lugha za Nuer na

Dinka. Baadae zinachezwa kwa jamii wanaoishi katika televisheni za muda na sauti zinachukuliwa na kucheza kwenye kituo cha taifa cha redio. Licha ya mpango huu kuwa katika hatua za kwanza, unatoa mfano mzuri wa mawasiliano kwa wale wasiojua kusoma na kuandika kama yule mwenzangu niliyekuwa nasafiri naye.

Kwa hayo, neno la kuchapishwa bado lina ubora wake halisi. Hata kwa wale ambao hawawezi kusoma, Gurtong Focus Magazine, jadala lake la kuvutia na yali-yomo, daima hutoa uchapishaji bora kwa watazamaji wake!

Jacob J Akol ni mkurugenzi/mhariri wa Gurtong – Mpango wa Amani na Chombo cha Habari



thamani za osiea

MAPENZI YETU

Mapenzi yetu ndio kichocho
cha kazi yetu.

Inaamsha ari ya kufanya kazi bunifu kwa akili zaidi. Uchu huu unatupatia nguvu zaidi, mabadiliko, na ustahimilivu wa kufanya kazi kwenye mazingira magumu na yenye changamoto, mapenzi yetu yanafanya tusimame bila woga na kuhimili hatari na kutokua na uhakika.

HAKI

Haki inawakilisha yote
tunavyosimamia.

Lengo letu ni kujakikisha kila mtu – kwa ujumla na sio kinadharia wanapata haki sawa kushiriki kikamilifu katika jamii na kupata haki na 'hakisawa' kutoka kwa serikali na jamii.

USAWA

Tunafanya kazi kwa msingi wa
binadamu WOTE wanahaki ya kupata
haki za msingi na kupata fursa sawa
na rasilimali.

Watu walioko kwenye makundi yaliyotengwa na wachache mara nyingi hunyanyapaliwa na kuteswa. Sisi huwapa usaidizi katika madai yao ya kupata haki za kibinadamu minghairi ya jinsia, rangi, kabila, dini, uzao, umri, ulemavu, muelekeo wa kijinsia, ama misingi mingine. Ukizingatia uenezi wa mifumo dume na mifumo ya kijamii amabyo inawakandamiza wasichana na akina mana, tunasimama kidete kufanikisha usawa wa kijinsia.

MSHIKAMANO NA UMOJA KAZINI

Sisi ni timu ambayo inafanya kazi kwa
ushirikiano na kwa umoja.

Uelewa wetu, uwajibikaji na ushirikiano umezalisha nguvu ya kufanya kazi kwa uhakika. Miingiliano yetu daima huwa ya adabu na endelevu. Tunafanya kazi yetu kwa utulivu na ucheshi mkubwa. Tunasimama na wafanyakazi wenzetu wakiwa na wakati mgumu.

UADILIFU

Uadilifu unamaanisha kufanya
tunayoyanena.

Tunawajibika na kujibu mienendo yetu (ya kutenda na kutotenda) kwa wote. Tunadumisha maadili mema na utaalamu wa hali ya juu katika miingiliano yetu. Kwetu sisi, uadilifu ni kujenga mahusiano halisi kupitia heshima na hali ya usawa.

UBUNIFU

NA UVUMBUIZI

Tunajipa changamoto kufikiria
tofauti – njia mbadala, mawazo
mbadala, ufahamu pamoja na washirika
– kupanua mipaka ya uwezekano.

Mabadiliko yanaweza kuja tu kwa kutafuta nafasi kwa ubunifu, na ikiwezekana kuwa tayari kuingia matatani. Tunapaswa kutoogopa kufeli wakati kuna fursa murwa ya mafanikio. Hakika, tunathamini mafunzo na ukuaji kiakili.


KUSHEHEREKEA UTOFAUTI

Tunasaidia katika jitihada za kusherehekea na kushajiisha nguvu za utofauti wetu na kukuza uelewano katika tofauti zetu.

Tunaishi kwenye jamii yenye watu wa kila aina watokao kwenye misingi tofauti, imani tofauti na mienendo tofauti ya maisha. "Ni sisi" kwa sababu "wao ni" and "wao ni" kwa sababu "ni sisi". Wetu wako pamoja nasi.



OSIEA
Inawezesha hata ndege
mdogo kuliko wote
kuimba juu ya mti



978-0-9838647-7-6